

Mafundisho Ya Madhehebu

**na Rod Rutherford
Mtafsiri John Makanyaaga**

www.kanisalakristo.com

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la Kwanza- Kanisa la Agano Jipy.

Utangulizi

1. Kuna makundi ya kidini 2054 katika nchi ya Marekani siku hizi
2. Kuna makundi yapatayo 5000 ya kiunabii
3. Agano jipy linadhihirisha kuwa kuna Kanisa moja tu. Efeso 4:4-6; 1:22,23
 - (a) Je! Likoje?
 - (b) Twaweza kulirejeza katika hali yake ya awali?

Mazungumzo.

- I. Kanisa la Agano Jipy lilijengwa kwa mpango maalum aliuagiza Mungu.
 - A. Mungu alimpa utaratibu Nuhu wa kujenga safina. Mwanzo 6:14-16, 22
 - B. Mungu alimpa Musa utaratibu wa kujenga Hema ya kukutania. Kutoka 25:9,40; Ebrania 8:5
 - C. Mungu alimpa Sulemani utaratibu wa kujenga Hekalu 1Nyak. 28:11-13
 - D. Mungu pia alitoa utaratibu wa kujenga Kanisa lake.
 1. utaratimu (Muundo) wa mafundisho. Rumi. 6:17
 2. Paulo alifundisha mambo yale katika kila Kanisa. 1 Kor. 4:17
 3. Alimwambia Timotheo kwamba "Shika kielelezo (Muundo) cha maneno yenye Uzima uliyoyasikia kwangu" 2Tim. 1:13
 4. Mpango huu wa kimungu ni Agano Jipy. Yuda 1:3; 2 Yohana 1:9-11.
- II. Kanisa la Agano Jipy lilijengwa katika Manabii.
 - A. Manabii walisema kuwa kanisa litajengwa wakati Mungu atakapomwaga Roho yake kwa wote wemye mwili. Yoeli 2:28-32; Mdo. 2
 - B. Walisema kuwa litaanzishwa wakati Warumi wanatawala. Dan.2; Mdo.2: 1-47; Luka 2:1-7; 3:1-2.
 - C. Walisema litajengwa wakati mataifa yote watakapokwenda juu mlimani kwa Bwana, na Neno la Bwana litaanza Yerusalem. Isa. 2:2-4; Mika 4:1-4; Mdo. 2:1-47.
- III. Kanisa la Agano jipy ulikuwa ni sehemu ya mpango wa Mungu wa milele. Efeso 3:3-11
- IV. Kanisa la Agano jipy lilijengwa na Yesu Kristo na alilinunua kwa damu yake mwenyewe.
 - A. Yesu Aliahidi Kwamba "Nitalijenga Kanisa langu" Mat. 16:13-20
 - B. Yeye pia ndiye msingi na jiwe kuu la Pembeni. 1 Kor. 3:11; Efeso 2:19-22.
 - C. Alimwaga Damu yake kwa ajili ya Kanisa. Mdo. 20:28
- V. Kanisa la Agano jipy lilikuwa na utaratibu maalum.
 - A. Yesu Kristo ndiye Kichwa cha Kanisa. Efeso 1:22-23; Kolosai 1:18; Mat. 28:18
 - B. Agano jipy, Neno la Mungu, Injili ya Kristo ni Katiba ya Kanisa la Agano jipy. Marko 16:15; Gal. 1:6-9, 2 Tim. 3:16-17; Ufunuo 22:18-19.
 - C. Kila Kusanyiko linajitegemea. Mdo. 14:23; Wafilipi 1:1; 1 Pet. 5:1,2
 - D. Wazee walichaguliwa ili kuliangalia kundi la kila walipokuwapo. Mdo. 14:23.
 1. Waliitwa pia Maaskofu au waangalizi. Mdo. 20:17, 28; Tito 1:5,7.
 2. Waliitwa pia wachungaji. Efeso 4:11; 1 Pet. 5:1-4
 - E. Wazee hao walipaswa kutimiza sifa Maalum. 1 Tim. 3:1-7; Tit.1: 5-9
 - F. Mashemasi walikuwa ni watumishi wa Kanisa. Filipi 1:1; 1 Tim. 3:8-13.
 - G. Wainjilisti, watumishi wa neno, walikuwa ni wahubiri wa Injili. Mdo. 21:8; Efeso 4:11; 2 Tim. 4:1-5.
- VI. Kanisa la Agano jipy lilikuwa na mpango maalum wa Ibada. Yoh. 4:24
 - A. Walikutana kila siku ya Kwanza ya Juma. Mdo. 2:1; Law. 23:15-20; Mat. 28:1; Marko 16:1-2; Luka 24: 1-3; Yoh. 20:1-2, 19, 26; Mdo. 20:7; 1 Kor. 16:1-2; Ufu. 1:10
 - B. Kanisa la Agano jipy walikula chakula cha Bwana kila siku ya kwanza ya juma. Mat. 26:26-28; Mdo. 20:7; 1 Kor. 11:23-34; Mdo. 2:42.

- C. Kanisa la Agano jipya waliabudu kwa njia ya sala. Mdo.2:42; 1 Tim. 2:1-8.
 - D. Kanisa la Agano jipya waliimba nyimbo za kumsifu Mungu. Efeso 5:18-19; Kolosai 3:16-17.
 - E. Kanisa la Agano jipya walijifunza na kuhubiri neno la Mungu. Mat. 28:19-20; Mdo. 20:7; 2 Tim. 4:2-4.
 - F. Kanisa la Agano jipya walitoa Changizo zao kila siku ya kwanza ya juma. 1 Kor. 16:1-2; 2 Kor. 8 & 9.
- VII. Kanisa la agano jipya lilikuwa Na Kazi tatu muhimu walizofanya.
- A. Kuhubiri Injili Kwa ulimwengu mzima. Mat. 28:19-20; Mark 16:15-16; Luke 24:46-47; 2Tim. 2:2; Kol. 1:23
 - B. Walifundisha waliokolewa. Mat. 28:20; Mdo. 20:7; Efeso. 4:12; Rum. 1:15; Ebr. 5:12-14; 2 Pet. 3:18
 - C. Waliwasaidia wenye shida, wote waaminio Na wasioamini Ili hali walisema matatizo Yao kwao. Mdo. 11:27-30; 2 Kor. 8 & 9; Gal. 1:2; 6:10; Yakobo. 1:27
- VIII. Kanisa la Agano jipya lilikuwa na Umoja.
- A. Hawakujumuika na aina yeote ya jumuia za Kimadhehebu kama CCT; TEC; WAPO nk.
 - B. Hebu fikiri kama ingekuwa Petro awe Mkatoliki; Paulo awe Mmethodist; Yohana awe Mpresbersteriani; Yakobo awe Mlutheri, Filipo awe mpentekoste nk. Unadhani maandiko yaliyoandikwa na hawa mitume yangekuwa na umoja? Na Yesu Je! Alipoomba hawa mitume wawe na umoja, na wao wakawa katika migawanyiko tungalisema kuwa kweli walihubiri na kunena mamoa kama walivyoagizwa kuwa na umoja?
 - C. Usemi “Makanisa ya Kristo” inamaanisha makusanyiko mbalimbali ya Kristo yanayonena mamoa na si kwamba inamaanisha wingi wa madhehebu tofauti yanayoonekana siku hizi. (Rum. 16:16)
 - D. Mitume walikataza kabisa mgawanyiko katika Kanisa la Agano jipya. 1 Kor. 10-13
 - E. Yesu aliomba kwamba Mitume na wale watakaosikia neno lake wawe na Umoja. Yoh. 17:20,21.
 - F. Waalimu wa uwongo mitume waliwadhihirisha kwa wakristo walivyo. Rumi 16:17,18; Tito 3:10,11; 2 Yoh.1:9-11.
- IX. Kanisa la Agano jipya walihifadhi maadili mema ya Kimungu.
- A. Mitume walikataza kabisa matendo ya mwili. Gal. 5:19-21. Wakristo wa Kanisa la kwanza walionywa kutoishi kwa kuutumainia mwili.
 - B. Wote ambao hawakuishi maisha ya utaratibu waliondolewa ndani ya Kanisa la Agano jipya. 1Kor. 5; 6:9-11; 2Thes. 3:6
 - C. Washiriki wa Kanisa walitambulika kwa matendo yao ya upendano wa ndugu kati yao. Mdo. 2:44,45; 4:34-37; Yoh. 13:34-35; 1 Yoh. 3:11; 16-18, 23;
- X. Kanisa la Agano jipya lilikuwa na matumaini Kwamba:-
- A. Uenyeji wao uko mbinguni na si duniani. Filipi 3:20,21.
 - B. Walisubiri kurudi kwa Yesu mara ya pili. 1 Thes. 5:1-11
 - C. Walikuwa ni wageni na wapitaji katika nchi hii. 1 Pet. 2:11
 - D. Walisubiri kupewa taji ya uzima kwa siku ya mwisho. 2 Tim. 4:6-8.
 - E. Wategemea “mbingu mpya na nchi mpya” 1 Pet. 1:34-5; 2 Pet. 3:13.
- XI. Kanisa la Agano jipya lilikuwa na mpango maalumu wa kuingiza waamini.
- A. Lazima mtu asikie Injili. Marko. 16:15; Heb. 11:6; Yoh. 6:44_45; Rum. 10:17

- B. Lazima mtu Aamini Injili. 1 Kor. 15: 1-4; Rum. 1:16; Yoh. 8:24; Marko 16,16.
 - C. Lazima mtu atubu dhambi zake. Luka 24:47; Mdo. 2:38; 3:19; 17:30,31.
 - D. Lazima mtu akiri mbele ya watu ya kuwa Yesu ni "Mwana wa Mungu". Mat. 10:32-33; 16:16; Mdo. 8:37; Rum. 10:9,10; 1 Tim. 6:12.
 - E. Lazima mtu huyu abatizwe (Yaani atoswe majini). Marko 16:16; 1Kor. 12:13
 - 1. Ubatizo huu ulikuwa ni kuzikwa majini. Rumi 6:3-5; Kol. 2:12; Mdo. 8:36-38
 - 2. Ubatizo huu ulikuwa kwa "ondoleo la dhambi". Mat. 26:28; Mdo.38.
 - 3. Ili kuwa ni kwa "jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu". Mat. 28:29.
 - 4. Ili kumweka mtu katika Kristo ambamo katika yeche baraka zote za rohoni zinapatikana. Efeso 1:3; Gal. 3:26,27.
 - 5. Unatuokoa sisi. 1 Pet. 3:20-21; Mdo. 22:16; Uf. 1:5; Marko 16:16.
 - 6. Ulikuwa ni ufufuo kwa waliotenda dhambi. 1 Yohana 3:4; Rumi 3:23; Mdo. 8:12.
- XII. Washiriki wa Kanisa la Kristo waliendelea kuwa na Yesu kama Wakiri, Kuhani mkuu na mpatanishi wao. 1 Yoh. 2:1-2; Ebr. 4:15; 1 Tim. 2:5.
- A. Waamini walipaswa kuungama dhambi zao ikiwa walianguka. 1 Yoh.1: 6-10.
 - B. Waamini walitubu dhambi zao mara walipotenda baada ya kubatizwa, si kwamba walibatizwa tena (Ubatizo ulikuwa ni mfano wa kuzaliwa kwa mtu, kwani mtu akishazaliwa na mama Je! Akikosa atarudi kuzaliwa tena)? Mdo. 8:22.

Hitimisho.

- 1. Mwanzoni kulikuwa na Kanisa moja tu, wala hapakuwepo aina yoyote ya madhehebu.
- 2. Wote waliokolewa (waliobatizwa) Walikuwa ni Washiriki wa Kanisa la Kristo.
- 3. Kanisa la Kristo lilijengwa kwa mpango ule wa Yesu mwenyewe na si mpango wa Kimadhehebu.
- 4. Nasi pia twaweza kujenga Kanisa kutokana na mpango huo wa Yesu na si wa kibinadamu (Kimadhehebu).

Maswali ya kujadili.

- 1. Kuna Makanisa mangapi yanapatikana katika Agano jipya?
- 2. Lini Kanisa la Bwana lilianzishwa?
- 3. Wapi Kanisa la Bwana lilianzishwa?
- 4. Nani ni Kichwa cha Kanisa?
- 5. Katiba ya Kanisa la Agano jipya ni ipi?
- 6. Nini kazi tatu za Kanisa la Agano jipya?
- 7. Ni mambo gani yanayohitajika ili mtu aingie katika Kanisa.
- 8. Kwa nini Mungu alitoa matendo ya kufanya kwa wanaoabudu katika Kanisa lake?
- 9. Nani wanaoangalia Kanisa la Agano jipya?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 2 – Uchunguzi wa Historia ya Kanisa.

Utangulizi.

- 1. Historia ya watu wa Mungu katika Agano la Kale ni Historia ya uaminifu, uasi na kurudia hali ya awali.
- 2. Hii ni pia ni sawa na Historia ya Kanisa.
- 3. Kinachofuata katika kujifunza Biblia, Historia ya Kanisa ni kitu cha maana kujifunza.

Mazungumzo.

- I. Kanisa Mwanzoni.
 - A. Lilijengwa na Yesu Kristo. Mat. 16:18
 - B. Lilianzishwa siku ya Pentekoste, labda 33 BK. Mdo. 2.
 - C. Neno la Mungu ni mbegu ya ufalme. Luka 8:11.
- II. Uasi ulitabiriwa.
 - A. Yesu alionya kuhusu manabii wa uwongo. Mat. 7:15
 - B. Paulo alionya kuhusu Waalimu wa uwongo. (1 Tim. 4:1-5).
 - C. Kuanguka kutoka kwenye kweli kulitabiriwa. 2 Thes. 2:1-10
 - D. Roho alinena kuhusu baadhi ya watu kuwa watajitenga na Imani. 1 Tim. 4:1-3.
- III. Uasi wa awali kutoka katika mpango wa Agano jipya.
 - A. Maendeleo kuhusu Upapa.
 1. Katika karne ya pili mzee wa Kanisa aliyekuwa akiongoza vikao vya wazee alianza kuitwa Askofu na wale wengine waliendelea kuitwa wazee tu.
 2. Baadaye kidogo Askofu wa mji mkubwa, Kanisa lile mashuhuri alianza kutawala juu ya Makanisa yale madogo.
 3. Katika karne ya nne, Mababa (Patriarchs) walitawala katika miji ya Rumi, Constantinople, Antiochia, Alexandria na Yerusalem.
 4. Katika mwaka 606 BK. Askofu mkuu wa Rumi aliyeitwa Boniface III alitangaza kuwa yeeye ni Papa wa ulimwengu (Katoliki) na akawa ndiye Papa wa kwanza.
 - B. Kuinuka kwa Ukuu (madaraja ya watawala kanisani).
 1. Mgawanyiko wa madaraja ulitokana na taratibu ya dini za Kiyahudi na kipagani zilizoendelea wakati ule.
 2. Wakati huu ikawa kwamba ni Kuhani (Padre) tu ndiye anayeweza Kuhubiri, kutoa Chakula cha Bwana, kubatiza, kufungisha ndoa au kuzika.
 3. Useja ulianzishwa na Papa Gregory VIII katika mwaka 1075 BK.
 - C. Ukiri na Mabaraza.
 1. Mabaraza yalianza mapema katika karne ya pili walipokaa kujadili matatizo yaliyojitekeza katika Kanisa wakati ule.
 2. Ukiri wa kwanza ulitungwa na baraza la Nikea katika mwaka 325 BK.
 - D. Ubatizo wa watoto wachanga.
 1. Mafundisho kuhusu dhambi ya asili yalianza katika karne ya pili walakini yalikazwa zaidi na Augustino.
 2. Mafundisho kuhusu dhambi ya asili ilipelekea kuanza kwa Ubatizo wa watoto.
 - E. Ubatizo wa kunyunyiza na kumwagia.
 1. Katika mwaka 251 BK, Novatian, aliyekuwa mgonjwa alimwagiwa maji akiwa kitandani.
 2. Katika mwaka 1311 BK. Baraza la Ravenna liliamuru kuwa Ubatizo wa kunyunyiza ni sawa na Ubatizo wa kutoswa.
 - F. Vyombo vya muziki na kwaya.
 1. Papa Vitaliano katika mwaka 660 ndiye mtu wa kwanza aliyeanzisha utumiaji wa vyombo vya muziki katika Ibada za Kikristo.
 2. Kama ilivyotokea Baadaye katika mwaka 1250 ikakubaliwa katika madhehebu ya kikatoliki.
 3. Katika karne ya nne, darasa maalumu la waimbaji liliuja kuwa kawaida katika Makanisa.
 - G. Misa.
 1. Misa maalumu ya komonio ilianza mnamo katika karne ya pili.

2. Komonio ya kwanza nayo ilianza mnamo karne ya kumi na mbili.
 3. Mkate kubadilika na kuwa mwili halisi wa Yesu ilianzishwa na baraza la Lateran mnamo mwaka 1215.
- H. Kumtuka Mariamu.
1. "Mariamu Mama wa Mungu" ilianza kutumika baada ya baraza la Efeso katika mwaka 431, hii ilitokana na Ibada ya wapagani wa Waefeso kuhusu Mungu wao Diana mama wa mabikira, na kwamba wapagani hawa wakaongoka na kuwa wakristo, wakaja na Imani yao.
 2. Mafundisho ya kuwa Mariamu alizaliwa pasipo dhambi ya asili yalianza rasmi mnamo mwaka 1854.
- I. Kutuka sanamu.
1. Iliaminika kuwa wafu watakatifu wangeweza kuwasaidia na hasa kwa kuwaombea waliohai.
 2. Hii ilipelekea mauzo makubwa ya Ibada ya wafu na sanamu.
- J. Sikukuu za kidini.
1. Sikukuu nyingi za Kiyahudi na kipagani ziligeuzwa kuwa za Kikristo.
 2. Baraza la Nikea lilitamka tarehe ya Pasaka mnamo mwaka 325.
- IV. Wapinzani wa Kanisa la Rumi.
- A. Orthodox ya Mashariki (Greek Orthodox) walijitenga na Rumi mnamo mwaka 1054
 - B. Petro Wado mnamo mwaka 1150, alitafsiri Agano jipywa na akapinga Kanisa la Rumi.
 - C. John Huss wa Bohemia alitaka watu warejee Biblia, alichomwa moto kwenye mtu na Kanisa Katoliki mwaka 1415.
 - D. John Wycliffe katika Uingereza alitafsiri Biblia katika lugha ya Kiingereza mwaka 1382; anaitwa Nyota ya asubuhi wa Matengenezo.
- V. Watu wa Matengenezo.
- A. Mnamo mwaka 1517 Martin Luther, mmonaki alikemea uuzaaji wa sanamu.
 - C. Walutheri walirithi ukiri wa Augsburg katika mwaka 1530 na ikawa ndiyo madhehebu ya kwanza ya Kiprottestant.
 - D. Ulrich Zwingli alikuwa mwana matengenezo Mswis alijali sana mfumo wa Agano jipywa.
 - E. John Calvin aliongoza matengenezo kutoka Geneva, alianzisha taasisi za kidini za Kikristo mwaka 1536.
 - F. John Knox Wesley alijaribu kufanya matengenezo katika Kanisa la uingereza badala yake akaanzisha madhehebu ya Presbyterian.
 - G. John Smyth alianzisha Madhehebu ya Kibaptist katika Mwaka 1611.
 - H. Katika mwaka 1739, John Wesley alijaribu kufanya matengenezo Kanisa la Uingereza (Anglican Church) badala yake akaanzisha Madhehebu ya Methodist.
- VI. Marejeo (The restoration) ya Kanisa la Kwanza.
- A. Mwanzoni mwa miaka ya 1800 watu walianza kutafuta kurudi katika Biblia, ili wampendeze Mungu kama ilivyokuwa Kanisa la kwanza.
 - B. Nia yao ilikuwa kurudia Kanisa la kwanza kuliko kufanya matengenezo yaliyosababisha madhehebu mengi yaliyokwisha kuundwa.
 - D. Viongozi muhimu waliongoza Marejeo haya katika nchi ya Marekani Walikuwa ni: Thomas na Alexander Campbell, Walter Scott, na Barton W. Stone.

Hitimisho.

1. Mtu ambaye hajifunzi historia ya Kanisa ni vyema kurudia na kuisoma tena.
2. Biblia ni sawa kwa kila nyakati na kila Mafundisho na kila jamii yapaswa kupimwa kwa kutumika Biblia.

Maswali ya kujadili.

1. Ni kitu gani muhimu cha kujifunza ambacho mkristo anapaswa kujifunza zaidi ya Biblia?
2. Papa wa kwanza aliiwta nani?
3. Ni Baraza gani la kwanza lililotengeza ukiri wa kwanza?
4. Mtu gani wa kwanza aliyeanzisha vyombo vya muziki kanisani?
5. Lini na nani alianzisha Ubatizo wa kunyuniza na kumwagia kuwa ni sawa na wa kuzamisha?
6. Nini maana transubstantiation?
7. Ni baraza gani liliamuru kuwa Mariamu kuwa ni mama wa Mungu?
8. Nani anaitwa "Nyota ya asubuhi" wa matengenezo?
9. Nani alilaumu mauzo ya sanamu?
10. ni madhehebu gani ya kwanza ya matengenezo (Protestant)?
11. Nani alianzisha madhehebu ya Kibaptist?
12. Nani alianzisha madhehebu ya Methodist?
13. Nini ilikuwa nia ya watu wa Marejeo?
14. Ni kitu gani kinachofaa kwa vizazi vyote?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 3- Ukweli na Mamlaka katika dini.

Utangulizi.

1. Watu wengi wanaamini kuwa ukweli unalingana.
 - (a). Wengine husema "si kitu, ikiwa mtu ataamini chochote kwa moyo wake wote itafaa tu.
 - (b). Wengine husema "wote tutakwenda Mbinguni, lakini kwa njia mbalimbali tofauti.
2. Swalii la msingi katika dini ni "Nini kitakachofaa kutuongoza na kuwa chenye mamlaka katika?
3. Hakuna kamwe umoja mpaka hapo kitu kinachofaa kutuongoza kwenye mamlaka ya dini kitakapo kubaliwa pamoja na wote wanaotaka umoja.

Mazungumzo.

- I. Zingatia hali halisi ifuatayo kuhusu Ukweli.
 - A. Ukweli waweza kufahamika. Yohana 8:32
 - B. Ukweli waweza kununuliwa (kupokelewa) au kuuza (kukataliwa). Mithali 23:23
 - C. Ukweli huweka huru, hutakasa, na husafisha. Yohana 8:31,32; 17:17; 1 Pet. 1:22.
 - D. Ukweli ni Lazima kuutii. 1 Pet. 1:22,23.
 - E. Ukweli ni Lazima kujizoeza. 2 Yoh. 1:4
 - F. Makosa (kinyume cha Ukweli) Lazima yakemewe. Gal. 4:16; 2:4,5.
 - G. Mtu anayetaka kuokolewa ni Lazima atii ukweli. 2 Thes. 2:10-12.
 - H. Kweli nini?
 1. Yesu ndiye kweli (Yeye ndiye chanzo cha ukweli wote, na asili ya kila kilicho halisi). Yohana 14:6
 2. Neno la Mungu ni kweli (Mungu amefunua, mamlaka, na uwezo wake kwa ajili ya mwanadamu). Yohana 17:17.
- II. Ni mamlaka gani yanastahili kukubaliwa katika Dini?
 - A. Mapokeo (Viapo) ya wanadamu? 2 Tim. 3:16,17.
 - B. Wazazi? Ezekiel 18:20; Rumi 14:12
 - C. Mkumbo wa watu wengi? Kutoka 23:2; Mat. 7:13,14.
 - D. Mhubiri, Mchubgaji au Kuhani? Mat.15:14; Yakobo 3:1; 1Yohana 4:1; 1 Wafalme 13:1-32.

- E. Kwa maoni na matakwa ya mtu mwenyewe binafsi? Waamuzi 21:25; Yeremia 10:23; 2 Wafalme 5:1-14.
- III. Ni Mamlaka gani pekee yenyeye nguvu ya kuwapeleka watu kwa Mungu?
- Neno la Mungu lililovuviwa na Roho wake. 2 Samueli 23:2; Isaya 8:20; Yeremia 1:9; 2 Tim.3:16,17; Gal. 1:6-9; 2 Pet. 1:20-21; 1 Thes. 2:13.
 - Neno hilo hairuhusiwi kubadili, kuongeza au kufanya lolote kinyume na lilivyoandikwa. Kumbukumbu 4:3; Mithali 30:5,6; Ufunuo 22:18,19.
 - Sisi sote tutahukumiwa kwa neno la Mungu katika siku ya Mwisho. Yohana 12:48; Ufunuo 20:11,12.

Hitimisho.

- Ukweli siku zote hudumu na uwongo hautadumu.
- Tunafahamu ukweli katika hisabati, kwa nini tusielewe ukweli katika neno la Mungu?
- Mafundisho yote na madhehebu Lazima yapimwe kwa neno la Mungu, ukweli ndio ufunuo wa Mungu.
- Tusipokubali mpango sahihi wa Mungu, kamwe hatukuwa na: umoja, kuokolewa au kumpendeza yeye kwa njia yoyote.

Maswali ya kujifunza.

- Swali la msingi katika dini ni lipi?
- Eleza mambo yanayofanya ukweli ueleweke.
- Ukweli ni nini?
- Ni mambo gani yanayokubalika katika mamlaka ya dini?
- Ni kitu gani kilicho hakika kitakachotupeleka mbinguni?
- Ni kitu gani ambacho ni kosa pamoja na Mapokeo (Viapo)?
- Kuna hatari gani kama tutafuata wahubiri, wachungaji au Kuhani?
- Ni nini kitawapata wale wote ambaao hawapendi kweli?
- nini kitatokea kwa wale wanaoongeza neno au kupunguza la Mungu?
- Nini kitacho tuhukumu siku ya Mwisho?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 4- Dhambi ya Madhehebu.

Utangulizi

- Kuna makundi ya kidini 2054 katika nchi ya Marekani siku hizi.
- Kuna makundi yapatayo 5000 ya kiunabii katika Africa
- Madhehebu ni nini?
 - Ni kikundi cha dini chenye jina na Mafundisho yaliyo tofauti na kikundi kingine cha dini ileile (kwa mfano makundi ya dini ya Kikristo yenyeye mfundisho yasiyopatana).
 - Hawaijiti Kanisa kwa ujumla isipokuwa ni sehemu tu nao huwa na sehemu inayobaki kuwa ni ya wanadamu.
- Kutokuwa madhehebu hutumika tu wakati madhehebu yote hayahusiki.
- Kutokuwa madhehebu ya kweli ni Kanisa lile tu la kweli mwili wote ukiokolewa, Kanisa halisi lilitofunuliwa ndani ya Biblia kabla ya madhehebu kuwapo.

Mazungumzo

- Je! Maandiko yanaunga mkono madhehebu?
 - Bwana anao kondoo wengine. Yohana 10:16.
 - Inamaanisha watu wa mataifa (Wasio wayahudi).
 - watakuwa kundi moja na zizi moja, mchungaji mmoja.

- B. Madhehebu ni matawi ya mzabibu? Yohana 15:1-3.
1. Yesu aliongea kwa wanafunzi wake siyo kwa madhehebu.
 2. Zingatia: anasema katika umoja (kila tawi siyo matawi).
- C. Madhehebu ni Washiriki wa mwili mmoja? 1 Kor. 12:12-27.
1. Mshiriki binafsi ndiye anaye zungumzwa katika fungu hili.
 2. fungu hili linafundisha umoja na si mgawanyiko.
- II. Maandiko yanapinga umadhehebu!
- A. Ni kosa kuchukua majina ya kibinadamu. 1 Kor. 1:10-13.
 - B. Magawanyiko, kikundi, faraka ni kazi ya mwili. Gal. 5:19-21.
 - C. Kuliita Kanisa la Bwana kuwa ni madhehebu hakuwezi kulifanya liwe madhehebu. Mdo. 24:5,14.
- III. Je mtu ye yeyote anaweza kuwa mkristo bila kuwa Mshiriki wa madhehebu?
- A. Wakristo wa kwanza waliitwa wakristo hata ingawa madhehebu hayakuwapo. Mdo. 2:47; 11:26.
 - B. Ni katika madhehebu gani yule towashi wa Ethiopia alikuwa Mshiriki?
 - C. Ikiwa kila mmoja atafuata maelekezo yale yaliyofuatwa na wakristo wa kwanza, ataongezwa pia katika Kanisa la Bwana kama vile walivyokuwa wale wa kwanza.

Hitimisho.

1. Biblia pamoja na Mapokeo ya wanadamu hufanya madhehebu moja.
2. Biblia pekee humfanya mtu kuwa mkristo tu.
3. Kwa kuutii Biblia siku hizi, kila mmoja wetu atakuwa mkristo na Mshiriki wa Kanisa la Kristo.

Maswali ya kujifunza.

1. Nini fafanuzi ya neno Madhehebu?
2. Je! Kuna madhehebu yoyote yanayoweza kudai kuwa ni mwili kamili wa Yesu leo?
3. Ni Kanisa gani Wasio madhehebu?
4. Jibu mjadala wa umadhehebu unaosimamia Yohana 10:16.
5. Jibu mjadala wa umadhehebu unaosimamia 1 Kor. 12:12-27.
6. Jibu mjadala wa umadhehebu unaosimamia. Yohana 15:1-7
7. Je Kanisa la Bwana ni madhehebu?
8. Je! Ni madhehebu gani yule Towashi wa Kushi alikuwa mshiriki?
9. Kama mtu leo atatii maandiko sawa sawa na watu wa karne ya kwanza walivyofanya, atakuwa mshiriki wa madhehebu gani?
10. Ni kitu gani ambacho kinamfanya mtu kuwa mshiriki wa madhehebu?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 5- Kutafuta Umoja.

Utangulizi.

1. Dini siku hizi ulimwenguni zimeganyika vibaya.
2. Yesu aliombea umoja. Yohana 17:20-21.
3. Magawanyiko yamekatazwa katika Agano jipya. 1 Kor. 1:10-13

4. Mambo mengi yaliyotofauti yamewekwa (yamebuniwa) na wanadamu yamewaondoa watu kwanye umoja.

Mazungumzo.

- I. Wengine humshukuru Mungu kwa kuwa ameleta magawanyiko.
 - A. Wanaamini kuwa Kanisa moja ni zuri tu sawa na lingine hajjalishi ni jinsi gani wametofautiana na wengine katika Imani zao.
 - B. Billy Graham wakati Fulani alisema: "Kuchagua Kanisa ni sawa na kuchagua kofia. Hata suti usiyotaka kunipa mimi, walakin kila mmoja atachagua ile anayoona kuwa ni bora kwake".
 - C. Wengine humfanya Mungu kuwa ndiye aliyeleta machafuko. 1 Kor. 14:33.
- II. Wengine hujaribu kuwa na umoja kwenye Matengano.
 - A. "Hufagia kwenye zuria"; mafundisho yao yote yanatofautiana na wao hukubaliana kutokubaliana.
 - B. wengine hawana umoja wa kweli.
 - C. Imedhihirika kwamba ni uwongo uliodhiri kudai wana umoja wa kweli.
- III. Mikutano ya maaskofu siku hizi hujaribu kuweka juhudu ya pamoja kuyaweka madhehebu yote yawe katika Kanisa moja kubwa.
 - A. Mafundisho hujadiliwa ili kutafuta muafaka kama vile wanasiwa wafanyakyo.
 - B. Baadhi ya juhudu zao huzaa magawanyiko zaidi.
 1. katika nchi ya Australia, Wamethodist, Wapresbyterian, na makusanyiko ya Makanisa yote yameungana.
 2. Lakini kwa upande Fulani kila kundi hukataa kufuata muungano huu.
 3. Matokeo yake yalikuwa Makanisa manne yalionekana katika makundi matatu.
- IV. Ni jinsi gani twaweza kuungama na kumpendeza Mungu?
 - A. Ni kwa njia ya kufuata Biblia bila kuongeza wala kubadili neno la Mungu, tunaweza kuwa na umoja wa kweli.
 - B. Wote wanaoamini na kutii Biblia moja kwa moja wao wameungana na wengine pia wanaoamini na kuutii Biblia.

Hitimisho

1. Magawanyiko kati ya wanaoamini katika Kristo ni kutoka katika neema na ni dhambi.
2. jibu halipatika katika Mikutano; makongamano, na muungano ya Makanisa bali ni katika kufundisha, Kuhubiri na kufuata neno la Mungu.

Maswali ya kujifunza.

1. Kwa nini Yesu aliombea umoja kwa waaminio kutokana na mafundisho ya Mitume kwamba wote wawe na umoja?
2. Kwa nini ni Makosa ikiwa "umoja katika magawanyiko" umetokea?
3. Kwa nini ni Makosa kumshukuru Mungu kwa kuleta magawanyiko?
4. Nini nia ya Mikutano ya Kimadhehebu ya maaskofu siku hizi?
5. Nini Makosa mawili ya muungano wa Kimadhehebu kwenye Mikutano yao?
6. Ni kitu gani muhimu kwa wanaoamini katika Kristo kinachowezza kutuunganisha pamoja ili tumpendeze Mungu?
7. Jibu la migawanyiko nini?
8. Ni kitu gani kinacho tuunganisha moja kwa moja?
9. Je! Agano jipya linakubali au linakataza magawanyiko?

Mafundisho ya Madhehebu.

Somo la 6-Kanisa la Roman Katoliki.

Utangulizi

1. Kanisa la Roman Katoliki lina tofauti aina tano.
 - a. Ni madhehebu ya zamani kuliko yote ulimwenguni.
 - b. Ni mama wa madhehebu yote duniani
 - c. Ni madhehebu kubwa kuliko zote ulimwenguni.
 - d. Ni madhehebu yenye nguvu kuliko yote duniani.
 - e. Ni madhehebu iliyotoka kwenye ukweli, ndiye waovu kuliko wote duniani.
2. Ni madhehebu iliyo na muundo wa utawala wa kisiasa wakati huo lina muundo wa kidini.

Mazungumzo.

- I. Asili na Historia yake.
 - A. Yesu, Paulo, Petro, na waandishi wengine walitabiri uasi mkuu kutoka kwenye kweli. Mat. 7:13-23; Mdo. 20:28-32; 2 Thes. 2:1-12; 1 Tim. 4:1-5; 2 Pet. 2:1-3; Yuda 1:3,4.
 - B. Paulo alisema kuhusu Kuanguka na Kuinuka kwa mtu mwenye dhambi. 2 Thes. 2:1-12.
 - C. Roho Mtakatifu alishudia kwamba wengine:
 1. Watazuia watu wasioe.
 2. Watazuia watu wajiepushe kula nyama. 1 Tim. 4:1-3
 - D. Kanisa Katoliki lilijiondoa katika Kanisa la Agano jipya na kuliharibu.
 - E. lilikuja kuwa Kanisa kubwa mno hasa wakati Boniface III alipojitungaza kuwa ndiye Papa wa Kanisa Katoliki mwaka 606 BK.
 - F. Liligawanyika mwaka 1054
 1. Magawanyiko yaliitwa ya kuvunja sanamu na kupinga matumizi ya sanamu katika Ibada.
 2. Kanisa la Mashariki lilipinga sanamu wakati lile la magharibi lilizikubali.
 3. Kanisa la Mashariki lilikuja kujulikana kama Orthodox ya Mashariki.
 - G. Matengenezo ya waprotestant katika karne ya 16 yavunja kongwa la ukatoliki ulikithiri katika magharibi.
- II. Ukweli walifundisha
 - A. Kuna Mungu mmoja katika nafsi tatu za Uungu.
 - B. Biblia ni neno la Mungu.
 - C. Waliamini kuwa kuna mbingu, kuzimu, kiama ya watu na hukumu.
 - D. Walipinga talaka na kuhimiza usafi wa maisha ndoa nyumbani.
 - E. Walithamini maisha ya binadamu na kupinga kutoa mimba na kuua kiumbe Bila kukiumiza.
- III. Makosa waliyofundisha.
 - A. Walifundisha kuwa wao ni ndio pekee Kanisa Katoliki la kimitume.
 1. Papa Boniface VIII, katika chumba maalumu kitakatifu; iliyotolewa mwaka 1302, taarifa yake ilisema kwamba, nje ya Kanisa Roman Katoliki, Hakuna kabisa wokovu wala ondoleo la dhambi. Baadaye alisema, “..... ni Lazima wote wanaotaka kuolewa, wanadamu wameumbwa wawe chini ya ukuhani wa Roma”. (angalia katika Eternal Kingdom, ukurasa 196).
 2. Ili Kanisa liwe Kanisa la kweli, ni Lazima likubaliwe na taratibu za mpango wa Agano jipya. Kanisa Katoliki halikubaliwi na Agano jipya.
 - B. Wanafundisha kuwa kuna sakramenti saba(mambo yaliyo sahihi kwa mtu anayetaka neema), hata ingawa neno sakramenti halipatikani katika Biblia. Sakramenti hizo ni:
 1. Ubatizo
 2. Kitubio
 3. Kipa Imara
 4. Ekaristi takatifu

5. Mpako Mtakatifu
 6. Daraja takatifu (Upadrisho)
 7. Ndoa.
 C. Walifundisha kuwa Mapokeo, amri za Papa na Mikutano mingine ya Kanisa yana mamlaka sawa na Biblia.
1. Ni kama mito miwili inayotirisha maji katika bustani ya Edeni, Biblia na Mapokeo ya Kimungu yana kamilisha neno la Mungu. Katika haya mawili ikiwa yanapingana, kwetu mapokeo bora na salama. (Catholic Belief, by J. faa Di Bruno, ukurasa 33).
 2. Biblia pekee hutupa sisi yote tunayohitaji kwa ajili ya wokovu. 2 Tim. 3:16,17; 2 Pet. 1:3; Yuda 1:3.
 3. Haturuhuswi kuongeza, kupunguza, au kwenda kinyume cha Biblia. Kumb. 4:2; Mith. 30:5,6; 2 Yoh. 1:9-11; Uf. 22:18,19; gal. 1:6-9.
 4. Kufuata mafundisho, amri na Mapokeo ya wanadamu ni kwenda kinyume cha neno la Mungu, na ni dhambi. Mat. 15:9,13,14.
 5. Mtu yejote anaweza kusoma na kuelewa Biblia yeye mwenyewe. Yohana 5:39; Mdo. 17:11; Efeso 3:3,4.
- D. Wanaamini kwamba Kanisa lijengwa juu ya Petro, kwani yeye ndiye mwamba. (Mt. 16:18)
1. Petro (Kefa) ni Jiwe (Yohana 1:42).
 2. Katika Mathayo 16:18, maneno yametumika kuonesha neno "Kefa".
 - a. Petros ($\pi\acute{\epsilon}\tau\rho\delta$) maana yake ni jiwe
 - b. na Petra ($\pi\acute{\epsilon}\tau\rho\alpha$) maana yake ni Mwamba, kanisa lilijengwa juu ya Petra (mwamba) na si ya Petros (jiwe).
 3. Mwamba ule wa Mathayo 16:18 ambao Kanisa lilijengwa juu yake ni ukweli ule ya kwamba "Yesu Kristo, mwana wa Mungu aliye hai" alioukiri Petro baada ya Yesu mwenyewe kuwauliza mitume kuwa yeye ni nani. Mat. 16:16; Mdo. 4:11,12; 1 Kor. 3:11; 10:4; Efeso 2:19-22; 1 Pet. 2:3-8.
- E. Wanafundisha kuwa Petro alikuwa Papa wa kwanza na alikuwa na nguvu za kusamehe dhambi, au kuondoa dhambi kama walivyo mapapa wao leo.
1. Petro aliahidiwa funguo za ufalme wa mbinguni na alizitumia kufungua ufalme kwa wayahudi siku ya Pentekoste na kwa mataifa alifanya hivyo katika nyumba ya Kornelio. Mat. 16:19; Mdo. 2 & 10.
 2. Uwezo wa kufunga na kufungua walipewa pia mitume wengine kama vile alivyopewa Petro. Mat. 18:18
 3. Kuna sababu saba zinazomfanya Petro asiwe kamwe papa:
 - a. Alikuwa mzee wa Kanisa sawa na wazee wengine na siyo Mzee mkuu wa wengine. 1 Pet. 5:1.
 - b. Alikuwa mwenye dhambi, mwenye uwezo kukosa kama wengine. Mat. 26:31-35, 69-75; Gal. 2:11-14.
 - c. Alikataa kusujudiwa. Mdo. 10:25-26.
 - d. Alioa mke na alitembea naye kwenye Kuhubiri. Mat.8:14,15; 1 Kor. 9:5.
 - e. Kristo ndiye Kichwa cha Kanisa. Efeso 1:22,23; Kol. 1:18.
 - f. Hakuna historia sahihi kwamba Petro alianzisha kanisa Rumi.
 - 1) Ni jambo geni, kama Petro alikuwa Rumi, kwamba Paulo hakuwezi kumtaja Petro alipoandika waraka kwa warumi. Rum. 16.
 - 2) Hata kama Mapokeo yangesema kuwa Petro aliwhi kuwa Rumi yangekuwa kweli, walakini inabakia kuwa Hakuna uhakika kuwa Petro alikuwa Papa.
- F. Wanamwabudu Mariamu.
1. Wanaamini kwamba Mariamu ni mama wa Mungu na ni mke wa Roho Mtakatifu.
 - a. Maandiko hayakuwahi kumwita kamwe kuwa ni mama wa Mungu.
 - b. Kama mume wake angekuwa Roho Mtakatifu, basi Mariamu alikuwa mzinzi maana angekuwa na waume wawili. Mat. 1:19,24.
 2. Wanaamini kuwa Mariamu ni mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu, lakini Yesu ndiye mpatanishi pekee. 1 Tim. 2:5

3. Wanafundisha kuwa Mariamu alizaliwa bila dhambi ya asili. Katika Biblia Hakuna kamwe fundisho kama hili. Rumi 3:23; 1 Yoh. 3:4; Ezekiel 18:20.
 4. Wafundisha kwamba alipalizwa mwili na Roho kwenda mbinguni. Ebr. 9:27; 1 Kor. 15:50; 2 Kor. 5:10.
 5. Yesu hakumweka Mariamu awe bora kuliko wengine. Yoh. 2:3-5; Luka 11:27-28.
 6. Wanafundisha kuwa Mariamu ni bikira milele, lakini Biblia inafundisha kuwa alikuwa na watoto wengine na alikuwa mke wa Yusufu. Mat. 1:24,25; 13:55,56; Yoh. 7:3-5; gal. 1:19; Yuda 1:1.
- G. Wanaamini watu waliokufa wakiwa watakatifu wanaweza kuwaombea wao.
1. Wanaamini kuwa watakatifu wanaweza kuondolea watu dhambi pia waliokufa nao wanaweza kuombewa na wa duniani wakasamehewa dhambi zao.
 2. Watakatifu wanaweza kusikia maombi ya waliohai na kuwasaidia.
 3. Hakuna mahali popote katika Biblia panafundisha hivyo, na ni kinyume cha mafundisho ya Kristo Kuhani wetu mkuu, Wakili na mapatanishi wetu na ni damu yake pekee inayowe3za kuondoa dhambi zetu. Ebr. 4:14-16; 1 Tim.2:5; 1 Yoh. 1:5-2:2.
- H. Wanawagawa watu katika matabaka ya watu wakawaida na wakuu.
1. Biblia haina matabaka.
 2. Wakristo wote ni makuhani. 1 Pet. 2:5,9;Uf. 1:6.
- I. Wanafundisha mafundisho ya tohorani (Purgatory).
1. Mkatoliki ambaye hakuwa mwema wakati ule alipokufa na hastahili kwenda mbinguni, basi huenda mahali pa mda ambapo atateswa mpaka dhambi zake zitakapokwisha.
 2. Tohorani si fundisho la Biblia.
 3. Wakatoliki husema kwamba sanamu zaweza kununuliwa ili kuwatoa wafu walioko katika mteso mapema kabla ya muda uliopangwa.
 4. Biblia hufundisha kuwa Hakuna nafasi kamwe baada ya kufa. Ebr. 9:27; Luka 16:19-31; 2 Kor. 5:10.
- J. Wanafundisha kuwa mkate na divai hugeuka kuwa mwili na damu halisi wa Yesu wakati Padre anaposoma misa ya meza ya Bwana.
1. Wakati Yesu aliposema "Huu ni mwili wangu" na pia "Hii ni damu yangu" alikuwa akitumia mfano (Mithali), kwani wakati huu alikuwa hajafa bado wala hajamwaga damu yake.
 2. Meza ya Bwana ni ukumbusho wa mwili na damu ya Yesu na siyo sadaka. 1 Kor. 11:24.
- K. Hawafundishi mpango wa wokovu.
1. Wanaamini kuwa wanadamu wanarithi dhambi ya asili. Kumb. 24:16; Ezekiel 18:19,20; 1 Yoh. 3:4; Yak. 4:17.
 2. Wanabatiza watoto. Rum. 10:17; Yoh. 8:24; mat. 10:32; Luka 13:3; Marko 16:15-16; Mdo. 8:12.
 3. Wamezoea kunyonyiza badala ya kutosa wanapobatiza. Rum.6:4; Kol.2:12; Mdo.8:36-39

Hitimisho.

1. Baraza la Trent lililokutana mwaka 1545 hadi 1563 liamuru kuwa mafundisho ya kikatoliki yana nguvu.
2. Mafundisho kwamba Papa hawezি kukosea yalianzishwa mwaka 1870, wakasema kuwa papa akiwa kwenye kiti chake cha enzi hawezی kukosa.
3. Mambo mengi ya kikatoliki yamerithiwa pia na wasio wakatoliki
 - a. Krismasi kama siku ya kuzaliwa kwa Yesu.
 - b. Kufunga kwaresma siku 40 kabla ya Pasaka.
 - c. Pasaka husherehekewa kama siku ya kufufuka kwa Kristo.
 - d. Watu wema tu ndiyo watakatifu. 1 Kor. 1:2; 6:11
4. Washiriki wa kanisa Katoliki wapata 825,000,000.

5. Wanayo Makanisa katika mataifa 217 duniani.
6. Mabadiliko mengi hufanywa mara nyingi katika kanisa la roman Katoliki.
 - a. Cardinali Gibbons alisema kuwa kanisa Katoliki ni taasisi isiyobadilika. (Faith of our Fathers P. 83).
 - b. Neno misa sasa limeingizwa kwenye lugha mbalimbali za watu.
 - c. Watu wa kawaida hupenda kuungama wakiwa wamekaa chini mbele ya kuhani kuliko maungamo alioagiza Yesu.
 - d. Kuna makundi makubwa ya yanayojitolea yanayotokana na wakatoliki yapata 300000.
 - e. Upinzani juu ya Useja umeenea, uzazi wa mpango na kutoa mimba.
 - f. Hivi sasa vyote mkate na divai hutolewa kwa Washiriki wote.
 - g. Kujizuai kula nyama siku ya ijumaa si muhimu siku hizi.

Maswali ya kujifunza.

1. Andika mambo matano yanayofanya roman Katoliki kuwa tofauti.
2. Nani aliyejitungazia kuwa yeye ni papa wa kanisa Katoliki kila mahali?
3. Katika mambo gani katika mwaka 1054 kanisa Katoliki liligawanyika?
4. Ni kitu gani kilivunja ukatoliki?
5. Je! Kanisa Katoliki lina kubaliana na utoaji wa mimba na mauaji yasiyo na maumivu?
6. Sakramenti ni nini? Neno hili linapatikana katika Biblia?
7. Andika sakramenti zote saba.
8. Ni kitu gani ambacho wakatoliki wanakilinganisha na Biblia?
9. Kanusha Usemi wa wakatoliki kwamba kanisa lilijengwa juu ya Petro.
10. Kanusha fundisho la Mariamu kuwa mama wa Mungu.
11. Elezea fundisho la kuzaliwa pasipo dhambi ya asili.
12. Eleza unavyofahamu kuhusu Ibada ya wafu.
13. Kanusha fundisho la makate na divai hugeuka mwili na damu halisi ya Yesu
14. Ni jinsi gani wakatoliki wanavyofundisha kuhusu Ubatizo? Je! Biblia inafundishaje?
15. Nini maana ya neno tohorani? Imefundishwa katika Biblia?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 7- Madhehebu ya Lutherani

Utangulizi

1. Madhehebu ya Kilutheri ndio madhehebu ya Kiprotestant ya zamani kuliko mengine.
2. Si moja bali kuna mengi yaliyotofauti katika Lutheri.
 - a. Kanisa kuu la Ujeruman, Denmark, Norway, Sweden na Finland yote ni ya kilutheri.
 - b. Kwa wakati mmoja kuna bodi zipatazo 150 za Kilutheri katika nchi ya Marekani.
3. Walutheri wamejaa hasa katika kaskazini na magharibi ya kati ya nchi ya Marekani.

Mazungumzo.

- I. Asili na historia ya Walutheri.
 - A. Martini Luther ndiye mwanzilishi wa madhehebu haya.
 1. Alizaliwa katika nchi ya Ujerumani mnamo mwaka 1483.
 2. Alikuja Baadaye kuwa mmonaki wa Ki-Augustino na alitafuta wokovu katika hali ya wema.
 3. Alisoma Biblia na kugundua kuwa mtu huhesabiwa haki kwa Imani.
 4. Alikuja kuwa msomi wa kiwango cha juu katika chuo kikuu, Kuhani (Padre) katika Parish, na aliwekwa wakfu katika Daraja lake.
 5. Katika mwaka 1517, alipinga mafundisho 95 yaliyohusu mauzo ya sanamu na mafundisho yasiyoendana na Biblia na aliyagongomea kwenye mlango wa kanisa huko Wittenberg ili Baadaye kuwe na mjadala, badala yake ilizusha tatizo baada ya rafiki yake kutafsiri kwa Kijerumani.
 6. Alikataa kutubu katika baraza huko Worms mwaka 1521 na alitengwa na kanisa Katoliki.

- B. Baadaye Luther akajulikana kama kiongozi wa matengenezo ya Kijerumani.
1. Alitafsiri Biblia katika lugha ya Kijerumani.
 2. Alielezea hasa kuwa waamini pia waweza kuwa makuhani, kuhesabiwa haki kwa Imani, maandiko ndio yenye mamlaka katika dini, na haki ya kila mtu kutafsiri Biblia mwenyewe.
 3. Aliamini kuwa kitu chochote kufanya chochote ambacho Biblia imekataza ni kosa.
- C. Katika mwaka 1530, ukiri wa Augsburg ulichukuliwa na Walutheri kuwa ni ukiri wa Walutheri, na ndio ukawa mwanzo wa madhehebu.
- D. Kundi la kwanza la wahamiaji wa Kilutheri walihamia nchini Marekani mwaka 1623, na kusanyiko la kwanza la Kilutheri lilikutana katika New York mwaka 1649.
- E. Miaka mingine 250, maelfu ya Walutheri kutoka ulaya walihamia katika nchi ya Marekani.
1. Mwaka 1870, kundi la nne la Kilutheri waliwasili Marekani.
 2. Inakisiwa kuwa kuna Walutheri 10,000,000 katika nchi ya Marekani siku hizi wakiwa makundi 12 tofauti.
- F. Kanisa la Kilutheri (Missouri Synod) lina washiriki idadi yao wapata milioni tatu.
1. Walifadhilli "Muda wa Walutheri"
 2. Katika miaka ya 1960 walijiingiza katika vita vya mageuzi na mageuzi ya ki-theologia, wakanza kulegeza mafundisho yao. (Mead, P. 1520).
 3. Matokeo ya hayo walipoteza Washiriki wao wapata 100,000.
 4. Wasomi wa historia ya Makanisa wanasema ni kwa mara ya kwanza kwa madhehebu kurudi kwenye ulegezaji na kuacha mafundisho ya msingi ya kanisa husika.
- II. Ukweli wanaoushikilia.
- A. Kawaida Wanafundisha ukweli kuhusu Uungu.
 - B. Wengi huamini maneno, yote yaliyovuviwa.
 - C. Wanafundisha kuwa ukuhani waamini wote ni makuhani, lakini kuna Daraja pia.
 - D. Wanafundisha kuwa Biblia ndiye mwenye mamlaka katika ukristo, lakini zipo ukiri kadhaa wanazozifuata.
- III. Ni mambo gani walutheri hufundisha kinyume cha Biblia?
- A. Wanayemwanzilishi wa kanisa Martini Luther badala ya Yesu. Mat. 16:18.
 - B. Kanisa hili lilianza mahali tofauti na pale palipotabiriwa na mahali pale Yesu alipoanzisha. Mdo.2.
 - C. Wanafuata ukiri wa Augsburg, ukiri wa Nicene, Ukiri wa mitume, Ukiri wa Athanasian, Ukiri wa Smalcald kitini cha Imani na mfumo wa amani na madhehebu mengine badala ya kufuata Biblia pekee. 2 Tim. 3:16,17.
 - D. Wanajiita walutheri kuliko kuijita wakristo. Mdo. 4:12; 11:26; 26:28; 1 Pet.4: 16.
 1. Luther mwenyewe alikataza kabisa akisema: "nawaomba ndugu zangu, muache jina langu pekee, kamwe msijiite wenyewe walutheri, bali wakristo". (Michelet, life of Luther P. 262).
 2. Wana jina lisilosahihi kwa kanisa maana Yesu mwenyewe ndiye mwenye kanisa na si Luther. Mat.16: 18; Rum.16: 16; 1 Kor. 1:2;Yohana 10:30.
 - E. Wanaendelea kushikilia amri kumi za Musa hata ingawa zimegongomewa msalabani. Kol. 2:14-15; 2 Kor. 3:7-11; gal. 5:1-4; Rum. 7:1-4.
 - F. Wanafundisha kuwa jumapili ni siku ya Sabato na kutunza Sikukuu nyingine kama vile Kwaresma, Pasaka, Christmas nk. Mdo, 20:7; 1 Kor. 16:2; Ufunuo 22:18,19; Kut. 20:8-11.
 - G. Wanafundisha kwamba Chakula cha Bwana ni sakramenti ambao katika hiyo msamaha wa dhambi unaweza kupatikana, (Lutheran Catechism P. 159), lakini Biblia inafundisha kuwa ni ukumbusho tu. 1 Kor. 11:24-26.
 - H. Wanafundisha kuwa mkate na divai hugeuka kuwa mwili na damu halisi vya Yesu. Mat. 26:26-28.
 - I. Wanafundisha kuhesabiwa haki kwa Imani pekee bila aina yoyote ya matendo ya Imani. (Catechism, p. 104)

1. Luther katika kutafsiri Rumi 3:28 aliongeza neno “pekee” katika Agano jipya. Uf, 22:18,19.
 2. Alisema kuwa yafaa waraka wa Yakobo uondolewe katika Agano jipya kwa sababu unaelezea kuwa Imani ni Lazima iambatane na matendo.
- J. Walutheri Wanabatiza watoto wachanga.
1. Wanasema kuwa watoto wamerithi dhambi miyoni mwao. Lutherani catechism p. 146).
 2. Kristo aliamuru kwamba watoto wadogo ni Lazima waletwe kwake na tunatii amri hiyo kwa kuwabatiza na kuwafundisha” (catechism p. 146).
 3. Kosa ni nini katika kuwabatiza watoto?
 - a. Watoto wachanga hawana dhambi, na wako salama. Eze. 18:20; 1 Yoh. 3:4 Marko 10:14.
 - b. Ubatizo ni Lazima ufuatwe na kusikia, kuamini Injili, kutubu dhambi, kukiria mbele ya watu na kasha kubatizwa. Mk. 16:15-16; rum. 10:17; Mdo. 2:38; Rumi. 10:8-10.
 - c. Katika Agano jipya wanaume na wanawake ndio walibatizwa. Mdo. 8:12.
- K. Walutheri wanamwagia na kunyunyiza wanapobatiza.
1. Kanuni moja ni nzuri tu kama nyingine (Yaani ukimtosa mtu au kunyunyiza Hakuna ubaya).
 2. Biblia hufundisha kuwa Ubatizo ni kuzikwa tu. Kol, 2:12; Rumi 6:3-5; Mdo. 8:36-39.
- L. Walutheri hufundisha kuwa Ubatizo umechukua nafasi ya kutahiriwa.
1. Tohara ilifanyika ikiwa ni ishara ya Agano; kwa hiyo watoto hubatizwa ili waingie katika agano jipya, ni muhuri wa haki katika Imani. (Small catechism question, 335).
 2. Tohara ya kimwili ilikuwa ni tohara ya kiroho. Rumi 2:28-29
 3. Kama tohara ilikuwa ni mfano wa Ubatizo, kwa nini wanaume tu walibatizwa?

Hitimisho.

1. Kwa sababu ya nia ya Martin Luther dhidi ya Biblia, Walutheri wameyachukua mambo mengi ya kikatoliki.
2. Walutheri pia wana muundo wa kiserikali. Efeso, 5:23; Mdo. 14:23.
3. Walutheri wanatumia vyombo vya muziki wanapofanya Ibada. Efeso 5:19; Kol, 3:16.
4. Walutheri ni wagumu kuokolewa kwa sababu ya mapokeo yao, jamii zaona wanakubali kuwa mapokeo yanaweza kuongezwa mahali pa neno la Mungu.

Maswali ya kujifunza

1. Nani ni mwanzilishi wa kanisa la Luhteri? Eleza maisha yake ya awali.
2. Eleza baadhi ya mafundisho ya Martini Luther.
3. Ni lini madhehebu ya Lutherani yalianza rasmi.
4. Ni kundi lipi la kilutheri lililojihusisha mageuzi katika miaka ya 1960?
5. Kwa nini ni Makosa kutumika jina la Luther?
6. Kwa nini Walutheri wanaamini kuwa amri kumi bado zina nguvu? Hii ni sawa? Kwa nini?
7. Ni nini mafundisho ya Walutheri kuhusu meza ya Bwana? Ni jinsi gani wanatofautiana na wakatoliki?
8. Kanusha fundisho la Walutheri kuhusu kupata wokovu kwa neema tu.
9. Kwa nini Walutheri Wanabatiza watoto wachanga?
10. Biblia inafundishaje kuhusu Ubatizo?
11. Kwa nini Martini aliongeza maneno ya Mungu?
12. Kwa nini Walutheri ni wagumu kupokea wokovu kufuatanana na mpango wa Agano jipya?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 8- Madhehebu ya Wapresbyterian

Utangulizi.

1. Wapresbyterian ni moja ya tawi muhimu Katika historia ya matengenezo ya kiprotestant.
2. Yalianzisha makusanyiko kwa maana ya kufanya matengenezo na matokeo yake yaanzisha Madhehebu.
 - a. Si kwamba kuna aina moja tu ya Madhehebu haya bali kuna Madhehebu mengi tofauti ya aina hii, angalau katika nchi ya Marakani kuna makundi tisa tofauti yanayojiita kwa jina hili.

Mazungumzo.

- I. Historia ya Upresbyterian
 - A. Wapresbyterian wanao waanzilishi wawili hasa wa Madhehebu haya.
 1. John Calvin ambaye Theogia ya matengenezo inamuhusu kwa kuanzisha Madhehebu haya pamoja na makanisa ya Hugenot.
 2. John Knox mwana matengenezo kutoka Scotland, alianzisha Madhehebu ya Kipresbyterian katika nchi ya Scotland.
 - B. Konx alikuwa mhubiri mzuri aliyempinga mfalme wa Uingereza, Kanisa la Anglikana, na wote waliokuwa wakifuata desturi za kanisa Katoliki.
 1. Aliongoza vita dhidi kujitenga kutoka katika Kanisa la Anglican kwa makanisa yote ya Scotland.
 2. Kupitia Oliver Cromwell, Wapresbyterian kwa muda fulani katika miaka ya 1600 walitawala serikali ya uingereza.
 - C. Mkutano wa Westminister ulikutana mwaka 1643-48.
 1. Mkutano huu uliunda katekesimo.
 2. Mkutano huu uliunda uatawala wa kipresbyterian kuwa wa kiserikali, (yaani waliweka watawala katika kanisa lao kama vile kanisa la Anglikana au romani katoliki).
 3. Mkutano huu uliunda ukiri wa westminister, ukiri huu ulifanyiwa marekebisho mwaka 1967.
 - D. Kimapokeo wanayahitaji sana mafundisho ya Kicalvin.
 1. Calvin alifundisha habari ya kurithi dhambi
 2. Mungu anahiari kumchagua ye yeyote katika wokovu
 3. Kulikuwa na mpaka katika suala la ondoleo (fidia) ambayo Mungu hufanya katika Yesu.
 4. Kuwapo kwa neema nyangi za Mungu katika wokovu.
 5. Ulinzi kwa watakatifu.
 - E. Wapresbyterian walikuja Marekani miaka ya 1600.
 - F. Walianzisha vyuo vingi na shule za kiseminar kama vile Princeton University na Union thological Seminari.
 - G. Matengano yalitokea baada ya kushindana kuhusu kuwaweka wakfu makasisi (yaani kuwekewa mikono kwa kasisi na Askofu, kwa usemi mwininge kama vile waroma wana kitu kinaitwa updrisho).
 1. Kanisa la Cumberland la kipresbyterian lilianzishwa mwaka 1810 katika Dickson, jimbo la Tennessee nchini Marekani.
 2. Waliwakubali wale viongozi ambao hawakuwa na elimu kubwa ilimradi walitimiza sifa waliwaweka katika daraja la ukasisi.
 3. Wako jumla ya 85000 katika makusanyiko 840.
 4. Wanaendesha chuo Bethel katika Mackenzie, jimbo la Tennessee na Seminary ya Memphis.

5. Kuna tawi jeusi linaloitwa Second Cumberland Presbyterian lenye wafuasi 20000, ambalo lilijitenga mnamo mwaka 1869.
- H. Katika mwaka 1861 kanisa la Presbyterian liligawanyika kuhusu utumwa.
1. Katika mwaka 1983 matawi mawili yaliungana na kufanya umoja katika nchi ya Marekani.
 2. Jumla yao ni wafuasi 3,100,000 katika jumla ya makanisa 12,000.
- I. Katika 1936 kundi la kaskazini (Scottish church) liligawanyika kuhusu ulegezaji (Liberalism).
1. J. Gresham Machen aliongeza upinzani kwa wote waliokana kwamba Mariamu hakuzaa akiwa bikira na pia kwamba Biblia imevuviwa na roho mtakatifu.
 2. Makundi mawili yenyе msimamo juu ya maadili ya awali yaliundwa. Kundi la kibiblia la Kipresbyterian lilikuwa na wafuasi 10,000 na lile lililoitwa Orthodox Presbyterian hili nalo lilikuwa na wafuasi 17,500.
- II. Ukweli wanaoufundisha.
- A. Kimapokeo wanatunza ukweli kwamba Yesu alizaliwa na bikira, wanapinga mtu kufa badala ya mwagine, kufufuka kwa Yesu kimwili, lakini baadhi yao hakubaliani na haya.
 - B. Wanafundisha umuhimu wa kuwa na maadili ya hali ya juu sana.
 - C. Wanaelewa kuwa kila kanisa Mahali lilipo ni lazima litawaliwe na wazee wa Mahali pale.
- III. Uwongo wanaoufundisha.
- A. Wanafuata mawazo ya Calvin kwamba watoto wanarithi dhambi (Eze. 18:20; Marko 16:16; Yoh. 3:16; Mdo. 2:36-47; 1 Kor. 10:2).
 - B. Makundi yanayo jaribu kufanya maadili ya Mungu kuwa ya kisasa, wana kwenda kinyume cha mambo muhimu ya Imani
 - C. Wana kiapo (Creed) cha kibinadamu (2 Tim. 3:16-17).
 - D. Wanaamini mawazo zaidi kuliko neon la Mungu lililovuviwa (Wanaamini wingi wa watu unataka nini), (1 Kor. 2:11-13; 2 Sam. 23:2).
 - E. Kimsingi wanafundisha kuwa mtu anaokolewa kwa Imani peke yake (Yak. 2:14-26; Gal. 3:26-27).
 - F. Wana muundo wa kiserikali kinyume cha Agano jipya.
 1. Kila kusanyiko lina wazee wake, hii ni sawa kwa mujibu wa serikali (Mdo. 14:23; Tito 1:5).
 2. Kila kundi limeundwa ki-presbyterian na si ki- Agano jipya.
 3. Presbyterian limeundwa kwa kufuata mikutano ya wakuu wa kanisa (synod) na kufuata muundo wa Agano jipya.
 4. Wana Mkutano mkuu wenye katibu mkuu (mtendaji) pamoja na msemaji wa kanisa ambaye ndiye anayetamka mafundisho muhimu yanayokubaliwa na kanisa pia kama kuna tatizo baada ya Mkutano kukaa na kuamua la kufanya, basi ndipo msemaji hutangaza maamuzi kwenda kwa watu wa chini.

Hitimisho.

1. Kuna tawi moja la wa Presbyterian, lile la kimatengenezo la kaskazini mwa Marekani, linalopinga matumizi ya vyombo vyaya muziki katika Ibada, wao huimba zaburi, nyimbo mabalimbali kwa kundi zima.
2. Wapresbyterian wote hubatizwa watoto na pia kunyuniiza wakati wanapobatiza (Rumi 6:4; Kol. 2:12)
3. Kanisa la ki-presbyterian la Marekani ndilo linaongoza mikutano yote ulimwenguni.

Maswali ya kujifunza.

1. Taja watu wawili muhimu ambao ni waanzilishi wa Madhehebu ya Presbyterian.
2. Eleza historia ya ukiri wa Presbyterian, na ni lini ulifanyiwa marekebisho?
3. Nini mafundisho makuu la Calvin?
4. Nani aliongoza vita dhidi ya ulegezaji mionganoni mwa Presbyterian ya kaskazini (Scottish)?
5. Ni nini maoni ya baadhi ya Wapresbyterian kuhusu maandiko kuvuviwa?
6. Wapresbyterian wanfundishaje kuhusu wokovu?
7. Nini maana ya neno Presbyterian?
8. Je! Wapresbyterian wanaungwa mkono na maandiko kuhusu kuwa na uongozi wa kiserikali? Kwani au kama sivyo kwa nini isiwe?

Somo la 9- Madhehebu ya Methodist.

Utangulizi

1. Kuna makundi 23 ya kimedhodist katika nchi ya Marekani
2. Kuna makundi zaidi ya waamini wapatao 13,000,000 katika kaskazini mwa Marekani na ni zaidi ya 18,000,000 ulimwenguni.
3. Hata ingawa yalianzia Uingereza, isivyotegemewa, ni wengi zaidi nchini Marekani kuliko Uingereza.
4. Ni Madhehebu ya siku nyingi, yanayokubalika, na kufahamika sana.
5. Kwa sababu ya sera za ulegezaji na Injili inayoangalia jamii inasemaje, umethodist umaelekea kufa kabisa siku hizi.
 - a. Ripoti kadhaa zinasema kuwa, wamethodist hupoteza waamini 75,000 kila mwaka.
 - b. Ni Madhehebu yenye bidii ya hali ya juu sana kwenye mikutano yao ya wakuu ya kila mwaka.

Mazungumzo.

- I. Mwanzo na historia ya Wamethodist.
 - A. John Wesley ndiye mwanzili wa Madhehebu haya.
 1. Alikuwa ni Muanglikana (Episcopalian) mwenye madaraka (ukuu), alikuwa mwana wa mtumishi wa Anglikana.
 2. Yeye na ndugu yake Charles, pamoja nao George Whitefield, waliunda kilabu takatifu katika Chuo kikuu cha Oxford katika mwaka 1729.
 3. Wanafunzi wenzao waliwaita Wamethodist (watu wa utaratibu) wakiwatania.
 - B. Katika mwaka 1735, ndugu zake Wesley walikuja nchini Marekani katika jimbo la Georgia.
 1. Charles ndiye alikuwa katibu mkuu katika Oglethorpe.
 2. John Alikuja kuhubiri katika India, lakini hakufanikiwa.
 3. walikuja kuungana na wamoravian na wanelewana sana katika mafundisho yao.
 4. Walirudi Uingereza miaka miwili baadaye.
 - C. Katika mwaka 1739, John katika huduma zake za kidini na alikuwa na fafanuzi za Luther kwa kusoma waraka wa warumi, moyo wake ulibadilika na kuamshwa upya, alichukulia fundisho hili la Martin Luther kama ndiyo wokovu wake.
 - D. Akina Wesley na Whitefield wlanza kuhubiri watu wa kawaida popote ilimradi watu waliwasikiliza.
 1. Kanisa la Anglikana halikuwapokea wala kukubalina nao katika mafundisho yao.
 2. Walijaribu kuhuisha upya kanisa la uingereza walakini walishindwa.
 3. Kusanyiko la kwanza la Ki-methodist lilianza mwaka 1739 mjini London Uingereza.
 4. Kanisa la ki-methodist halikujulikana mpaka mwaka 1791.
 - E. Baada ya mapinduzi ya ki-marekani, Wesley alimchagua Francis Asbury na Thomas Coke kuwa wasimamizi wa kanisa la Methodist nchini Marekani.

1. Kanisa la Methodist lilikuwa haraka kutokana na mahubiri ya mzunguko ya wahubiri wake, theologia rahisi, na umsho mkuu ulioambatana na wahubiri hawa.
 2. Katika siku za mwanzoni, wamethodist walitambulika kwa hali yao ya kusisimuka kwao kama wanavyofanya wapentekoste.
- F. Kanisa la ki-methodist liligawanyika mwaka 1845 kuhusu tatizo la utumwa.
1. Katika mwaka 1939, matawi ya kaskazini na kusini yaungana na kufanya umoja wa ki-methodist.
 2. katika mwaka 1968, Kanisa la kiinjili la umoja wa ndugu nao walijiunga.
- G. Kanisa la umoja la ki-methodist lina waamini 9,482,000 kwa makusanyiko 37,000 siku hizi.
- II. Ukweli wanaofundisha.
- A. Wanafundisha kwamba Krsito alikufa kwa ajili ya watu wote.
 - B. Wanamini kuwa mtu wana hiari.
 - C. Wanafundisha kuwa mtu aliyekwisha okolewa anweza kuanguka.
 - D. Wanafundisha utakatifu wa mtu binafsi na uhusika binafsi wa mtu kwa Mungu.
 - E. Kwa siku zilizopita waliamini kuwa Biblia pekee ndiyo yenyenye mamalaka kuliko wao.
- III. Ni mambo gani wamethodist hufundisha kinyume cha Biblia?
- A. Wana kitabu cha Kanuni cha kibinadamu kinachowaongoza ambacho kinaitwa “Methodist Discipline”, yaani nidhamu ya ki-methodist (2 Tim. 3:16-17).
 1. Kama kuna katekesimo inachukua nafasi ya Biblia, imekwenda kinyume cha mapenzi ya Mungu.
 2. na kama inachukua nafasi ya Biblia kudogo basi itakuwa imekwenda kinyume cha Mungu kidogo.
 3. Na kama Biblia itachukua nafasi yote kwenye Imani, basi itakuwa imefaa kwa vyote.
 - B. Wana mwanzilishi wa kibinadamu, naye ni John Wesley (P.7, Discipline UMC 1976), Math. 16:18.
 - C. Wanashikilia utaribu ambao haukuandikwa (Mdo. 14:23; Filipi 1:1).
 1. Wana mikutano 73 kila mwaka ya kutunga sheria.
 2. Kati ya hiyo mitano ni ya kisheria ambayo hukutana baada ya kila miaka mine.
 3. Kuna mikutano ya maaskofu ipatayo 59 kwa idadi, inayokutana angalau mara moja kwa ujumla ili kuangalia na kuhamasisha ukuaji wa kanisa lao.
 - D. Katika kitini chao namba 9 kuhusu nidhamu walifundisha kuwa “tunaokolewa kwa imani peke yake, ni fundisho la muhimu kwa ujmla na linalifariji kwa wote kiroho”. (p. 57, the book of Discipline of the UMC 1976).
 1. Biblia hufundisha kwamba kuna matendo ambayo mtu anaweza kutenda mabayo hayana lolote katika wokovu wetu.
 - a. Matendo ya sheria ya Musa (Rumi 3:28; Gal. 2:16; 3:9-10).
 - b. Matendo ya mtu mwenyewe anayojitakia Ef. 2:8-9; Tito 3:4-5).
 2. Biblia hufundisha kuwa kuna matendo ambayo ni muhimu sana kwa ajili ya wokovu wetu kwa sababu yaliagizwa na Mungu ili tuyatende (Mdo. 10:34-35).
 - a. Ni lazima tumtii (Mat. 7:21-23; Lk. 6:46; Ebr. 5:8-9; Rum. 6:16-18).
 - b. Imani inaendana na matendo (Yak. 2:14-26; Gal. 5:6).
 - c. Imani yenyepeke yake imeitwa matendo (Yohana 6:29).
 - E. Wamethodists hufundisha kuwa kanisa lina matawi mengi na hivyo wao ni Sehemu ya matawi hayo: wanasema hivi “Kanisa la Methodist ni kanisa la Kristo... kanisa hili ni kuu sana katika waprotestant.. Mwanzilishi wake ni John Wesley”. (Book of Discipline of UMC, 1976 p.7)
 1. Biblia hufundisha kwamba Kristo ndiye aliyeanzisha kanisa moja tu (Mat. 16:18).

2. Biblia hufundisha kwamba kuna kanisa moja tu (Ef. 1:22-23; 4:4; 5:23).
- F. Wamethodist hutumia jina lisilo la kimaandiko (ni la kibinadamu) (P. 20, Discipline, 1976). Isa. 62:2; Mdo. 4:12; 11:26; 26:28; Rumi 16:16; 1 Pet. 4:16.
- G. Wamethodist hubatizwa watoto (p. 64 and 114; Discipline, 1976).
1. Biblia hufundisha kwamba mtu lazima asikie, aamini, atubu na aungame dhambi zake kabla ya kubatizwa, hakuna hata mtoto mmoja anayeweza kutimiza masharti hayo (Rumi 10:17; Marko 16:16; Mdo. 8:37; Rumi 10:10; Mdo. 2:38; 17:30-31; 8:12).
 2. Watoto wachanga hawajapotea, hawajawahi kufanya dhambi, wao ni salama (Mat. 18:1-3; 19:13-15).
- H. Wamethodist hunyunyiza humwagia na hutosa wanapobatiza, hata hivyo ubatizo wanaotumia mara nyingi ni wa kumwagia; Biblia hufundisha kuwa kuna ubatizo mmoja tu nao ni kutosa majini tu ndio uliokuwepo tangu mwanzo (Rumi 6:4-5; Mdo. 36-38; Kol. 2:12). Angalia Mead, P. 163.

Hitimisho

1. Kanisa la kimethodist lina mwanzili asiyeh sahihi, Mahali lilipoanzishwa hapakuwa sahihi na Tarehe lilipoanzishwa haikuwa sahihi, jina nalo si sahihi, muundo wake na njia za watu kuijunga nalo ili liwe kanisa sahihi kufuatana na Biblia hayo yote hayakuwa sahihi, kwa hiyo; halina haki ya kuendelea kuwepo (Mat. 15:13).
2. Ajabu ni kwamba mshiriki wao anaweza kuamini lolote au imani yoyote na akaendelea kuwa mmethodist.

Maswali ya kujifunza.

1. Ni wapi Madhehebu ya Methodist yalianzia?
2. Ni wapi liliopata nguvu na kukua haraka?
3. Kwa nini kanisa la ki-methodist linakufa siku hizi?
4. Nani alianzisha Madhehebu ya Methodist?
5. Walipata wapi jina lao?
6. Ni mwaka gani Kusanyiko la kwanza lilikusanyika kwa mara ya kwanza? Wapi?
7. Kwa nini kanisa la kimethodist lilikuwa haraka sana katika Marekani ya kaskazini?
8. Kitabu cha kanuni cha ki-methodist kinaitwaje?
9. Kuna kosa gani kwa mtu kutumia kitabu cha kanuni za kibinadamu?
10. Kulingana na kitabu cha wamethodist cha kanuni zao, mtu anaokolewaje?
11. Kanusha fundisho la kuokolewa kwa imani peke yake bila matendo.
12. Ni matendo gani ambayo hata kama mtu akitenda hayana maana kwa wokovu wetu?
13. Ni matendo gani ambayo ni muhimu kwa wokovu?
14. Wamethodist wanabatizaje? Kanusha ubatizo wao.
15. Kwa nini kanisa la ki-methodist halina haki kuendelea kuwepo?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 10- Madhehebu ya Baptist.

Utangulizi.

1. Kundi kubwa kabisa la kiprotestant katika nchi ya Marekani ni kanisa la kusini la ki-baptist lenye washirika 14,000,000.
2. Si kwamba kuna kundi moja tu la ki-baptist, lakini yapo jumla ya 27 tofauti ya kimadhehebu na mengi yanayojitegemea kote Marekani na duniani.
3. Jumla ya washirika wa Madhehebu haya yalikuwa 29,000,000 katika mwaka 1983 katika Marekani peke yake tu.
4. Wengi wa wabaptist wamekuja kuwa washirika wa kanisa la Bwana kwa urahisi kuliko Madhehebu mengine.

Mazungumzo.

- I. Chanzo na historia ya wabaptist.
 - A. Wengi wa wabaptist hudai kuwa Yesu Kristo ndiye mwanzilishi wa kanisa lao, na lilianzishwa katika siku za Yohana Mbatizaji.
 - B. Kundi moja wapo la kiprotestant katika matengenezo ya karne ya kumi na sita lilikuwa ni Anabaptist.
 - 1. Walipinga ubatizo wa watoto wachanga na waliwabatiza tena kama walivyofanya kwa watu wazima
 - 2. Anabaptist wa kwanza walikuwa wakinyunyiza, baadaye walianza kutosa.
 - 3. Walipinga adhabu za kiserikali, kutumika jeshini, kuapishwa, kulipa kodi, na waliamini kuwepo kwa tofauti kati ya serikali na kanisa kwa njia yoyote.
 - 4. Wamenonites (wafuasi wa Menno Simons) walitokana na Anabaptist.
 - C. Kundi la waingereza waliojitemba likiongozwa na John Smythe na Thomas Helwys, walikimbia kutoka Holland kuepuka mteso.
 - 1. Walikuja pamoja na wamenonite na walielewana sana wao kwa wao.
 - 2. John Smythe alibatizwa tena pamoja na wenzake wengi, na kuanzisha kanisa a Baptist.
 - 3. Tarehe ya kuanzishwa kwa kanisa la kibaptist inaanzia miaka ya 1607 mpaka 1609, au 1611, Kulingana na historia mbalimbali.
 - D. Kusanyiko la kwanza la Baptist lilianzishwa nchini Marekani na Roger Williams katika eneo la Rhode Island, mwaka 1639.
 - 1. Magawanyiko yalianza kutokea kutokana na Ucalvin na Arminians.
 - 2. Katika mwaka 1814 liliundwa kundi la kimishieni la kimageuzi katika Madhehebu ya baptist lilianzishwa.
 - E. Migogoro ilizuka hasa kati ya wale wabaptist wa kaskazini na kusini kutokana na kutofautiana kuhusu utumwa na muundo wao.
 - 1. Katika mwaka 1845 wabaptist wa kusini walijiondoa na kuunda mageuzi ya kusini ya kibaptist.
 - 2. Wabaptist wa kusini wana mafundisho yasiyobadiilika kuliko wale wa kaskazini (yaani wale wa kusini wanapinga ulegezaji kuliko wale wa kusini).
 - 3. wale wa kaskazini walibadli jina lao na kuitwa American Baptist (yaani Baptist ya ki-marekani) mwaka 1950.
 - F. Kundi la muungano wa undugu wa kibaptist (Baptist alliance) uliundwa mwaka 1905.
 - 1. Hivi sasa wapo washirika zaidi ya milioni 34.
 - 2. Kundi hili ndilo linalokubalika ambalo hukubaliwa na wabaptist wengi.
- II. Ukweli wanaofundisha.
 - A. Kwa ujumla wanatunza sana imani kwamba maandiko yamevuvuviwa na roho mtakatifu, hata ingawa wanavyo vitabu vya kanuni mbalimbali, walakini wanasema kuwa mamalaka kuu ipo kwenye Biblia.
 - B. Wengi wao huamini kuzaliwa kwa Yesu na bikira na kufufuliwa kwa Yesu kimwili.
 - C. Wale wenyewe msimamo wa kale hukataza hata vyombo vya muziki kwenye Ibada, na wafanya ukumbusho wa meza ya Bwana kila siku ya kwanza ya juma (jumapili).
 - D. Wabaptist wote wanaamini kuwa ubatizo ni wa kutoswa tu, na wanakataza kubatiza watoto.
 - E. Wabaptist wanapinga uovu na wanahimiza Maisha ya utauwa.

- III. Ni mambo gani wabaptist wanayofundisha yaliyo kinyume cha Biblia?
- A. Grover Stevens, aliyekuwa mbaptist alikisia kuwa 85% mpaka 90% ya wabaptist hawajui hakika ni nini hasa kanisa lao linafundisha.
- B. Baadhi ya wabaptist hufundisha kwamba kanisa lao lilianzishwa siku za Yohana Mbatizaji.
1. Yohana Alikuja kutayarisha njia ya Bwana (Yoh. 1:19-27).
 2. Yohana hakuwamo katika ufalme (Mat. 11:11).
 3. Ahadi ya kujenga kanisa ilitolewa baada ya Yohana Mbatizaji kufa (Mat. 14:10; 16:18).
 4. kanisa lilianzishwa siku ya Pentekoste (Isa. 2:1-4; Yoeli 2:28-32; Dan. 2; Mdo. 2).
 5. Yohana alibatiza kwa toba liletaloo ondoleo la dhambi, lakini wabaptist wa kisasa wanabitizwa kwa sababu dhambi zao zimekwisha samehewa (Marko 1:4).
- C. Wabaptist hufundisha kwamba kanisa si muhimu kwa wokovu.
1. Wanaamini kwamba mtu anaweza kuokolewa nje ya kanisa na kisha akajiunga na kanisa.
 2. Mtu anaweza kuokolewa hata si mshiriki wa kanisa la baptist, kwa hiyo; kanisa la ki-baptist si muhimu kwa wokovu.
 3. Biblia hufundisha kuwa kanisa ilikuwa ni Sehemu ya kusudi la Mungu la milele, na ilinunuliwa kwa damu yake; na kwamba ataliokoa kanisa lake (Ef. 3:8-11; Mdo. 20:28; Ef. 5:23).
 4. Biblia hufundisha kwamba kuwapo katika Kristo baraka zote za rohoni hupatika katika kanisa lake, na ikiwa mtu amewekwa ndani ya Kristo, basi amewekwa ndani ya kanisa (Ef. 1:3; 2:16; 1 Kor. 12:13; Gal.3:17).
- D. Wabaptist hufundisha mpango wa wokovu ambaa haapatikani kabisa katika Biblia.
1. Kwa ujumla hufundisha kwamba mtu anaweza kuokolewa kwa imani peke yake, lakini Biblia hufundisha kwamba tunaokolewa kwa matendo na si kwa imani peke yake (Yak. 2:24). (Angalia Hiscox Manual, p. 62).
 2. Hufundisha kwamba toba huja kabla ya Imani wakisimamia katika Marko 1:15; lakini wakati mwininge maelezo yao hayasimamii mpangilio wa Mdo. 5:3; kama mtu hutubu kabla ya kuamini Injili, toba haiwezi kuwa ni Sehemu ya Injili kwa sababu, toba hii huja kabla ya kusikia ijnili (Rumi 10:17); ni jinsi gani mtu anaweza kutubu ikiwa hajajua au kuamini kwamba Mungu amemwamuru kutubu?
 3. Kwa ujumla hufundisha ungamo la uwongo—wao husema “Naamini kwamba mateso ya Kristo yameondoa dhambi zangu”.
 - a. Hili halionekani katika Biblia
 - b. Inaelezea mafundisho ya uwongo—kwamba mtu huokolewa bila ubatizo kwa sababu wokovu uliumbwa kabla ya Ubatizo.
 - c. Hakuna ukiri rahisi wa imani katika Kristo aliye mwana wa Mungu unaopatikana katika Biblia (Mdo.8:37; lunganisha na uf. 22:18,19).
 4. Hufikiria kwa kipiga kura kama mtu ambaye ameokolewa kama anaweza mshiriki wao, jambo hili ni geni kabisa katika neno la Mungu Uf. 22:18,19; Gal. 1:6-9).
 - a. “Wakati makanisa wanatamani kupokea washiriki, wanakuwa na shaka kwamba wasije wakapokea mtu ambaye si mwema. Maknisa haya huwa na wagombea nafasi ya kuwa washirika wanaowajia, hutengeneza maneno kama haya, wape usoefu kwanza, na mapokezi yao hufanywa kwa kupiga kura ya kumkubali au la ili awe mshiriki. Ajabu ni kwamba anaweza kuwa mshiriki bila kubatizwa, badala yake kura ya wajumbe yaweza kumwingiza katika ushirika wao sawa na kumbatiza” (Hiscox Baptist Manual, p. 22).
 - b. Je! Waweza kufikiria ikiwa Petro angepigisha watu kura siku ya Pentekoste? Ni wapi katika maandiko tunapopata mfano wa aina hii? (Mat. 15:9)
 5. Wanafundisha kuwa ubatizo si muhimu kwa wokovu, ni kinyume kabisa na jinsi Biblia inavyofundisha: “Biblia hufundisha ni lazima kufanya kama ilivyokuwa siku za mitume, kwamba kulikuwa na Bwana mmoja, Imani moja, na ubatizo mmoja, na hakukuwa na Madhehebu tofauti yaliyokuwapo siku zile, ubatizo unaokoa ndio ule tu uliokuwa unawaingiza watu ndani ya kanisa, na ni njia hii tu ilimpa haki mtu kuwa mshiriki wa kanisa.” sasa ni tofauti kabisa hata hayo...” (Hiscox Manual p. 22).
 6. Nini Biblia husema?

- a. Ubatizo unatuokoa (Mk. 16:16; 1 Pet. 3:21).
- b. Ubatizo ni kwa ondoeo la dhambi (Mt. 26:28; Mdo. 2:38).
- c. Ubatizo unaosha dhambi Mdo.22:16; Uf. 1:5).
- d. Ubatizo hutuingiza katika Kristo ambapo hupokea baraka zote za Mungu (Ef. 1:3; Gal. 3:26-27).
- e. Sijawahi kusoma Mahali popote katika Agano jipya baada ya siku ya Pentekoste ambapo mtu akiokolewa bila kubatizwa.
- f. Biblia hufundisha kwamba tunazikwa kwa njia ubatizo (Rumi 6:4).
- g. Ubatizo si jambo la kufanyika mara nyangi kama wasemavyo wabaptist, bali ni jambo linalotendeka mara moja tu.

E. Wabaptist hufundisha kwamba, mtu akiokolewa mara moja basi amekwisha okolewa haanguki tena.

1. Biblia hufundisha kwamba, Mtu anaweza kuamini akaokoka na kuanguka tena (Lk. 8:13).
2. Mtu anaweza kuanguka kutoka kwenye neema ya Mungu (Gal. 5:4).
3. Paulo alihofia sana kwamba huenda akaanguka na kuwa mtu wa kukataliwa (1 Kor. 9:27).
4. Tumeonywa kwamba “tuangalie tusije tukaanguka” 1 Kor. 10:12).
5. Ukaidi (kufanya dhambi kwa jeuri) husababisha mtu kuanguka (Ebr. 10:26-27).
6. Simoni mchawi aliamini, na baadaye alianguka (Mdo. 8:13-22).
7. Yakobo alifundisha kwamba mtu anaweza kukosa katika kweli, na kisha akaokolewa na kutoka katika hatari ya kifo (Yak. 5:19-20).
8. Paulo alifundisha kwamba wengine watajitenga katika imani (1 Tim. 4:1).
9. Petro alifundisha kwamba “mtu akianguka akatoka kwenye kweli, hali yake ya pili huwa mbaya zaidi kuliko ile ya kwanza” (2 Pet. 2:20-22).
10. Mafundisho yale ya kusema kwamba, hili likisha tokea halitakuwa vile kama vile Shetani alivyomwambia Hawa kwamba hamtakufa, yalianza tangu zamani (Mwa. 3:4).

Hitimisho.

1. Ubatizo (isipokuwa ule wa kwanza) wa kutoswa huku ukutumia vyombo vya muziki wakati wa Ibada haisaidii katika wokovu (Ef. 5:19; Kol. 3:16).
2. Ubatizo wa kutoswa ni kosa ikiwa unaambatana na wanaoabudu bila kuchukua chakula cha Bwana kila siku ya kwanza ya juma (Mdo. 20:7).
3. Ubatizo wa kutoswa ni makosa ikiwa utaambatana na watu kutumia majina ya kibinadamu (Isa. 62:2; Mdo. 1126; Rum. 16:16).
4. wengi hukosa hata ingawa hubatiza kwa kutosa walakini wanajaribu kurekebisha maneno ya Mungu yawe ya kisasa, na kufuata mafundisho ya Calvin ambayo huwaongoza watu kwenye upotevu, uasi, kama vile kusema kuwa kuna dhambi ya asili, miujiza nk.
5. Watu wengi (si wote) hufundisha kimakosa kwa kujaribu kuwaeleza watu habari za millennia.

Maswali ya kujifunza.

1. Ni Madhehebu gani iliyokubwa zaidi katika nchi ya Marekani?
2. Ni ubatizo za aina ngapi walizonazo Madhehebu?
3. nani alianzisha Madhehebu ya kwanza ya Ki-baptist?
4. Nani alianzisha Kusanyiko la kwanza katika nchi ya Marekani, lini?
5. Ni ukweli upi ambao ubatizo huwa nao kuhusu wokovu?
6. Kanusha fundisho kwamba Yohana Mbatizaji alianzisha katika.
7. Ni ubatizo upi unaokubaliwa sana watu? Je Ubatizo wa Biblia ukoje?
8. Kanusha fundisho la wabaptist linalosema kwamba, Kanisa halina kazi yoyote katika wokovu wa Mtu.
9. Kwa nini ni vigumu kwa mtu kutubu kabla ya kubatizwa?
10. Wabaptist wanasemaje kuhusu ubatizo? Je! Biblia inasemaje kuhusu ubatizo?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 11- Wanafunzi wa Kristo na kanisa la kikristo huru.

Utangulizi.

1. Makanisa ya Kristo na wanafunzi wa Kristo/ Kanisa la kikristo lililohuru walishiriki pamoja na wale waliokuwa wakijaribu kurejeza kanisa katika hali yake ya awali ilivyokuwa katika Agano jipya.
2. Wanafunzi wa Kristo, pia huitwa Kanisa la kikristo, na ni kanisa la kikristo lililohuru, pia hujulikana kama kanisa la (“Conservative”) wanaolinda mambo ya kale, kundi ambalo lina washiriki wachache sana siku hizi.
3. Kwa sababu wana desturi zinazofanana kihistoria, tunajifunza pamoja kwa hawa wanaoitwa wanafunzi na kanisa huru.

Mazungumzo.

- I. Chanzo na historia yao.
 - A. katika miaka ya mwanzoni mwa 1800, watu wa Madhehebu ya mbalimbali walianza kuhimiza watu kurejea kwenye Biblia.
 - B. Baadhi ya watu hawa walikuwa:
 1. Elias Smith na Abner Jones wakiwa uingereza.
 2. James O’klley katika Virginia na Carolina ya kaskazini.
 3. Barton W. Stone katika Kentucky.
 4. John Wright wa Indiana.
 5. Thomas na Alexander Campbell katika Pennsylvania na Virginia ya magharibi.
 6. Chester Bullard wa Virginia.
 7. Herman Dasher wa Georgia.
 8. Walter Scott wa Ohio.
 - C. Baadhi ya mambo waliyotetea yalikuwa kama ifuatavyo:
 1. Katekisimo (Mapokeo) za wanadamu hazitakiwi kuongoza wanadamu, bali ni Biblia tu.
 2. Wakristo wako chini ya Agano jipya tu siku zote.
 3. Kanisa la Agano jipya laweza kupatika tu kwa wale wanaofuata Agano jipya.
 4. Waamini wasijiite majina ya kibinadamu.
 5. Umoja unapendeza na unawezekana tu ikiwa mfumo wa kanisa utakuwa kama ilivyokuwa katika Agano jipya
 6. Tunaweza kuwa wakristo kama walivyokuwa wakristo wa kwanza ikiwa tutafuata mpango wa wokovu ule uliokuwa katika Agano jipya.
 - D. Kundi hili lilikuwa haraka sana, na hesabu iliyofanywa mwaka 1850 ilioneshwa kuwa idadi yao walikuwa ni wa nne katika idadi ya watu katika wa Madhehebu kwa taifa la Marekani.
 - E. Kuanza mwanzo, walikuwa na makusudi mawili katika mpango wao.
 1. Walitaka kila mmoja ajihusisha na umoja wa waamini.
 2. Jambo la pili kujitahidi kurejeza kanisa katika hali yake ya awali (yaani ya Agano jipya).
 - F. Hii pia inaelezea mambo mawili tofauti dhidi ya Biblia.
 1. Walegezaji: (Liberal) Wao hujihuisha na mambo yale yaliyokazwa waziwazi tu kwenye Biblia, lakini kama halioneckani wazi kukatazwa, kwao ni halali (Kwa mfano, Biblia haisemi usinywe, basi wao hawamzui mtumiaji wa kileo, kosa ni kulewa si kunywa).
 2. Wale wenye msimamo wa kufuata mambo ya awali (Conservative): Wao husema, chochote ambacho Biblia, haitoi mfano wowote, au kama haieleweki, basi kwao kufanya jambo hilo ni kosa.

- G. Ishara ya kugawanyika iliokea katika mwaka 1849 wakati jumuia ya kimishieni ya ki-marekani ilipoundwa:
1. Ilitokana na umuhimu wa kuhubiri kwa ulimwengu.
 2. Wapinzani walidai kwamba kila Kusanyiko ni lazima lijhusishe binafsi kuhubiri Injili na ndiyo wao wanaopaswa kuwa wamisheni wa Mungu na si kuunda shirika la kimishieni.
- H. Katika mwaka 1859, vyombo vya muziki vikaongezwa katika Ibada.
1. Waliona kuna umuhimu wa kuboresha uimbaji.
 2. Wapinzani walisema kuwa kuimba kwa vyombo vya muziki ni kuongezwa neno la Mungu.
- I. Ubatizo kwa ajili ya ondoleo la dhambi ulielezewa kwa makini na tangu mjadala wa Campbell-McCalla katika mwaka 1823.
1. Katika mwaka 1837, mwanamke mmoja katika mji wa Lunnerburg, alimwandikia Alexander Campbell kwamba katika Madhehebu yote kuna wakristo pia huko nako.
 2. Katika kujibu, Alexander alisema: "Hakuna sababu, ikiwa kutoswa kumetendeka, kufuatana na utaratibu wa imani, ataokolewa na kufanyika kuwa mkristo...."
- J. Mgawanyiko kati ya walegezaji na watu wenye msimamo mkali ulijulikana rasmi katika hesabu ya mnamo mwaka 1906.
1. Walegezaji walijulikana kama wanafunzi wa Yesu Kristo au Kanisa la Kikristo; wanashirikiana na makundi mengine katika kazi ya kimishieni, wanatumia vyombo vya muziki katika Ibada nk.
 2. Wale walio na msimamo wa awali (Conservatives) Wanaendelea kushikilia kusudi lao la awali la kurudia hali ya kanisa la Agano jipy, hawa huitwa Kanisa la Kristo.
- K. Mageuzi ya ki-theologia yalianza kuwa fanya walegezaji kujulikana zaidi katika miaka ya mwanzoni mwa 1800.
1. R.L. Cave wa Kanisa la Kikristo la Central katika St. Louis mwaka 1889 alikana kwamba Yesu alizaliwa na bikira, ufufuo wa Yesu kimwili, na alielezea kwamba Biblia ni kitabu cha kinachobadrika (Evolution), na siyo kweli kwamba kimevuvuwa na roho wa Mungu, ufunuo.
 2. L.L. Pinkerton alitoa kipeperushi chake kilichokana mfumo wa zamani wa kuamini kwamba maandiko yavuvuwa na Roho.
 3. Karatasi iliyoitwa "Gombo" ilitolewa na msomi kijana, mhubiri, ilitetea waziwazi uanachama wake kwamba ni mwanachama wa mageuzi ya ki-theologia.
 4. Baada ya J.W. McGarvey kufa, waamini wa Biblia waliondolewa kabisa katika kitivo Biblia katika chuo cha Biblia badala yao wana mageuzi wa ki-theologia wakachukua nafasi. (Angalia Christians Scholar but Choate & Doran).
- L. Muda mfupi baada ya wanafunzi kujitenga kutoka makanisa ya Kristo juu ya vyombo vya muziki, ushirika wa kimishieni, walianza kugawanyika tena kuhusu mageuzi ya ki-theologia. (angalia Christians Only by Murch).
1. Walegezaji wa hali ya juu (Ultra Liberal) waliteka vyuo vingi muhimu, vyama mbalimbali na taasisi mbalimbali.
 2. Kwa kadiri wale wenye msimamo walivyozidi kusogea mbali na ukengeufu, ndivyo zaidi sana walivyozidi walegezaji nao walivyoendelea kuacha ukweli katika vyama vya kimishieni na vyombo vya muziki.
- M. Vita iliendelea kwa katibu miaka 50, lakini mpaka leo kanisa la Kikristo limegawanyika katika makundi mawili ya kimadhehebu tofauti.
1. Walegezaji wa hali ya juu wao huitwa "Wanafunzi wa Kristo, na
 2. wale wenye msimamo mkali huitwa "kanisa la Kikristo liilohuru".
- II. Wanafunzi wa Kristo.

- A. Wanafunzi hawa wanafanana sana na Wamethodist katika mwonekano wao wa kawaida karibu kwa kila kitu na kama mshiriki wa upande wowote akiingia upande mwingine anapokelewa kama mshiriki wao wa kawaida.
- B. Katika mwaka 1968, makubaliano kwenye mukutano katika mji wa Kansaa, walijenga uhusiano wa kindugu kwa karibu zaidi.
 - 1. Kusanyiko lao moja linakusanya mikoa ipatayo 35.
 - 2. Kuna mukutano wa wakawaida kwa ajili ya kuunda sheria.
 - 3. kuna boi maalumu inayohusika na mambo ya uhusiano na Madhehebu mengine.
- C. Ni wanachama katika baraza la Makanisa kitaifa na kimataifa, na wanajihuisha kwa ndani na mikutano ya kidini na Madhehebu mengine.
- D. Wana waamini 1,160,000 katika makusanyiko 5,000 katika nchi za Marekani na Canada.
- E. Wana jina lisilo la kimaandiko, utaratibu, Ibada na njia ya kuijunga, na uhuru wa kushirikiana na Madhehebu kinyume cha maandiko.
- F. Wako mbali sana na mpango wa kurejea katika kanisa la Agano jipya.

III. Kanisa la Kikristo lililohuru:

- A. Ndugu zetu pia huwaita hawa watu ni wenye msimamo wa kale (Conservative Christian Church) Kuwatofautisha na wale wanaoitwa wanafunzi.
 - 1. Katika maeneno ya kaskazini Wanajiita kanisa la Kristo (kwa kujitambulisha au kujilinganisha).
 - 2. Kwa ujumla wanaamini Uungu wa Yesu na kuvuviwa kwa maandiko.
 - 3. Wanajitahidi kuhimiza kurudia hali ya kanisa walakin wanatafsiri katika hali ya ulegezaji sana.
 - 4. Wanakiri kuwa ubatizo ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi, lakini wanawapokea watu wengine wa Madhehebu mengine ambao wametoswa kama ikitokea akitaka kuijunga nao.
- B. Makosa wanayofundisha.
 - 1. Wanatumia vyombo vya muziki na kwaya (Ef. 5:19; Kol. 3:16; Uf. 22:18-19). wanashirikiana na watu ambao hawakubatizwa kimaandiko (Mdo. 2:38; Ef. 5:11).
 - 2. Wanakuwa na bodi ya wazee na mashemasi na wanamwita mhubiri wao mchungaji (Mdo. 14:23; Filp. 1:1; 1 Tim. 3).
 - 3. wanawaruhusu wanawake kutumika katika Ibada (1 Tim. 2:8-15).
 - 4. Wanaamini habari za millennia, na kwamba ufalme bado haujadhihirika bado (Mt. 16:18-19; 1 Kor. 15:23-27).
 - 5. Huchukua chakula cha Bwana hata siku zisizo siku ya kwanza ya juma (Mdo. 20:7).
 - 6. Wanakuwa na wazee ambao hajatimiza sifa za ki-maandiko (1 Tim. 3; Tito 1).
 - 7. Katika baadhi yao hufundisha kuwa imani pekee kama njia ya wokovu (Mdo. 2:38; Mk. 16:16; 1 Pet. 3:20-21).
 - 8. Wana jumuia za kimishieni (Ef. 3:10,21; Mdo. 14:23).
- C. Kanisa la Kikristo lililohuru lina washiriki 1,000,000 katika makusanyiko 5,500.
 - 1. Wana vyuo 32 na vyuo vya ulegezaji vya kisanaa (Milligan) na vyuo vya juu vya ki-theologia.
 - 2. Nguvu zao hasa ziko upande wa majimbo ya katikati ya magharibi kama vile Ohio, Indiana, Kentucky, Missouri na Iowa katika nchi ya Marekani.
 - 3. Nyumba yao maalumu inayowatangaza hasa ipo Cincinnati katika Marekani.

Hitimisho.

1. Juhudi mbalimbali za kuunganisha Makanisa ya Kikristo na Makanisa ya Kristo zimeishia kushindwa kwa sababu zifuatazo:
 - a. Misimamo tofauti dhidi ya Biblia.
 - b. Kushindwa kuangalia zile tofauti na kuziondoa.
2. Wanafunzi watatoweka baada ya siku si nyingi zijazo kwani wanazidi kupungua kutokana na ulevezaji uliokithiri.
3. Kanisa la Kikristo lililohuru kimsingi ni Madhehebu ya kiinjili; wana hitaji kusikia na kuitii ijnili sawa na Madhehebu mengine wanavyitajika.

Maswali ya kujifunza.

1. Kuna tofauti gani kati ya Kanisa la Kikristo la wanafunzi na lile lililohuru?
2. Ni nini ilikuwa ishara ya Magawanyiko wakati wa mpango wa kurejea kanisa ulipokuwa katika nguvu?
3. Ni lini hasa Mgawanyiko ulijulikana rasmi kati ya kanisa la wanafunzi na kanisa lililohuru? Nini zilikuwa sababu kuu?
4. Nini lini kikundi cha mageuzi ya ki-theologia kiligeuza mpango wa kurejea kanisa?
5. Lini kanisa la wanafunzi na lililohuru watengana?
6. Ni nini baadhi ya makosa ya kanisa lililohuru?
7. Ni aina gani ya utaratibu wanaofanya wanafunzi wa kikristo? Ni lini hayo yote yalianza? Ni lini hasa walipokamiliika katika uanzishaji wao?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 12- Kanisa la Assemblies of God (Mkusanyiko wa Mungu)

Utangulizi.

1. Kuna zaidi ya washiriki milioni kumi wa kanisa hili katika ulimwengu.
 - a. Washiriki 1,900,000 wanakutana katika makusanyiko 10,000 katika nchi ya Marekani.
 - b. Wanao washiriki milioni 8 katika makusanyiko 85,000 katika nchi 105 za mataifa mbalimabli.
2. Ndiyo Madhehebu kubwa kuliko yote kati ya Madhehebu ya kipentekoste.
 - a. Kutoka mwaka 1970-1980 walijipatia washiriki 250,000 katika nchi ya Marekani pekee.
 - b. Katika muda huo huo walionegeza mara dufu washiriki katika dunia yote.

Mazungumzo.

- I. Chanzo na historia ya kanisa la Assemblies of God.
 - A. Nia yao ilikuwa kufanya uamsho ule ulianzishwa katika miaka ya 1800 na 1900.
 1. Mkutano wa sala ulifanyika katika chuo cha Biblia cha Bethel katika Topeka, Kansas mwaka 1901 ulizaa madai mengi ya wengi kusema wamebatizwa kwa Roho mtakatifu.
 2. Kundi kubwa la uamsho lilifuatia katika Azusa St. Mission mjini Los Angeles, jimbo la California, nchini Marekani.
 3. Makundi mengi ya kipentekoste yalikuwa kutoka katika maamsho hayo.
 - B. Katika mwaka 1914, wapentekoste 300 kutoka majimbo 20 katika nchi ya Marekani na baadhi ya nchi mbalimbali walikutana katika Hot springs, huko Arkansas.
 1. Walijishirikisha katika ushirika ulioitwa Mkutano mkuu wa makusanyiko wa Mungu (The general Council of the Assemblies of God).
 2. Katika mwaka 1916 walitengeneza mafundisho maalumu waliyoyaita ya ukweli ambayo ndiyo yamekuwa katekisimo yao.

- C. Makao makuu yao yapo Springfield, jimbo la Missouri nchi Marekani.
- D. Serikali yao uko kwa visehemu vifuatavyo:
1. Kila Kusanyiko lina kamati ya mashemasi ambao huchagua mchungaji na kuangalia mambo ya kanisa lao.
 2. katika nchi ya Marekani imegawanywa kila wilaya ina baba ambaye anaangalia, anatoa kibali, na kuwasimika wachungaji, pia anafadhili makanisa mapya katika wilaya yake.
 3. Baraza kuu hukutana kila baada ya miaka 2; na wakati huu husimika watumishi na kupata taarifa za kila Kusanyiko, pia hili ndilo baraza lenye uwezo wa kutunga sheria.
 4. Wakati baraza lao halipo kazini, wajumbe 200 wa bodi wanaoitwa mababa wanahusika na kazi hiyo ya baraza.
 5. Baraza kuu lina wajumbe watendaji 13 mababa ambao Huchukua maamuzi makuu juu ya utendaji wa kanisa.
 6. Katika utawala wa kanisa la Assemblies kuna mwangalizi mkuu, mwangalizi msaidizi, katibu mkuu, na mweka hazina mkuu ambaye anaelekeza kila siku kuhusu shughuli za fedha za Madhehebu hiya.
- E. Wanaendesha vyuo 9 vya Biblia, kati ya hivyo kimoja ni cha ulegezaji, na pia wana chuo kikuu cha juu cha kitheologia.
- F. Wana gazeti lao ambalo hutolewa kila wiki, lenye mzunguko wa nakala zipatazo 300,000
- G. Wana kipindi katika radio kila wiki kinachoitwa “muda wa uamsho” kinaruka katika vituo 570.
- H. Wanasaidia wamishenari 1230 wa kigeni na 317 wa nyumbani.
1. Bajeti yao kwa ajili ya wamishenari wa kigeni wanagharimu \$48,500,000 kwa mwaka.
 2. Wamishenari wa ndani wanagharimu \$10,500,00 kwa mwaka.
- II. Ukweli wanaofundisha.
- A. Wanaamini utatu wa Mungu katika Uungu.
- B. Wanaamini kuzaliwa na Bikira kwa Yesu na kufufuliwa kwa mwili kwa Yesu.
- C. Wanaamini maandiko, yakwamba Biblia imevuviwa.
- D. Wanaamini kuwa ubatizo pekee wa kimaandiko ni wa kutoswa.
- E. Wanaamini kwamba mtu anayohiyari kuchagua kufanya mema au mabaya.
- F. Wanaamini kuwa wakristo hawako chini ya Agano la kale na hawashiki amri za Agano la kale mpaka pale inaporudiwa kwenye Agano jipy.
- G. Wanafundisha kwamba mwana wa Mungu anaweza kuanguka kutoka kwenye neema.
- III. Ni mambo gani ambayo assemblies wanafundisha kinyume cha Biblia.
- A. Wanafundisha kwamba ubatizo wa roho mtakatifu bado upo ni unafanyika kwa wote wanaoamini hata siku hizi.

1. "Maandiko yanafunua kuwa hili ni jambo la kawaida kwa wakristo na kufundisha kwamba kila mwamini ni lazima atafute na kutegemea ubatizo huu. Ushahidi wa kwanza muhimu kwamba umepata ubatizo huu, ni kunena kwa lugha za zisizofahamika." (Who we Are and we Believe, p. 21, 22).
 2. Biblia inafundisha kuwa:
 - a. Ubatizo wa Roho matakatifu ulikuwa ni ahadi, siyo amri (Mat. 3:11; Yoh. 14:26; 16:7-13).
 - b. Ilikuwa ni ahadi kwa Mitume na ni wao tu waliopokea siku ya Pentekoste (Lk. 24:49; Mdo. 1:4-5; 26; 2:1-4, 14-21).
 - c. Nyumba ya Kornelio walibatizwa ubatizo huo kuthibitishia wayahudi kwamba mataifa nao wamekubalika kwenye injili sawa na Wayahudi (Mdo. 10:44-47; 11:15-17).
- B. Wanaamini kwamba karama zote za roho zilizotolewa kwa kanisa la mwanzoni, bado zinaendelea kutolewa katika kanisa hata leo.
1. "Tunaamini uponyaji ni moja ya habari njema ambayo Mungu anayo kwa ajili ya ulimwengu na kwamba Mungu anawaponya wagonjwa siku hizi kama ilivyokuwa katika siku za Biblia " (Who we Are and we Believe, p. 22).
 2. Biblia inafundisha kwamba:
 - a. Karama ya miujiza, ukijumlisha uponyaji na kunena lugha za kigeni kimiujiza, ilikuwa ni kuthibitisha Uungu wa Yesu na kulithibitisha neno la Mungu kuwa ni kweli (Yoh. 3:2; 20:30-31; Mk. 16:17-20; Ebr. 2:3-4).
 - b. Kwa kuwa neno limekwisha funuliwa na kuthibitishwa, karama za miujiza haihitajiki tena (1 Kor. 12:1-10; 13:8-13; Yak. 1:25).
- C. Wanafuata katekismo ya wanadamu wakiongeza katika Biblia.
1. Ilitungwa katika mwaka 1916 na iliitwa maelezo ya kimsingi yaliyo kweli (Statement of fundamental truths).
 2. Biblia pekee inatosha haturuhusiwi kuongeza wala kupunguza (2 Tim. 3:16,17; 2 Pet 1:3).
- D. Wanatumia vyombo vya muziki wanapofanya Ibada, walakini hakuna mamalaka yoyote inayowaruhusu kufanya hivyo katika Agano jipya (Ef. 5:19; Kol. 3:16; Uf. 22:18,19).
- E. Wana matabaka mbalimbali ya utawala ambaa ni mgeni kabisa katika maandiko.
1. Makao makuu ya kanisa la Assemblies yako katika Springfield Missouri, lakini kanisa la Kristo makao makuu yake yapo mbinguni.
 2. Wanao mashemasi na wachungaji waliowekwa kwa kila Kusanyiko, lakini mpango wa Mungu kwamba wazee (Maaskofu) na mashemasi wako juu ya kila kanisa (Mdo. 14:23; Filp. 1:1; 1 Pet. 5:1-4).
 3. Wanao maafisa wa ki wilaya na kitaifa, lakini Kristo ni kichwa cha kanisa zima ulimwenguni (Ef. 1:22-23; 5:23; Kol. 1:18).
- F. Kwa maoni yao na si kwa kanisa bali ki Madhehebu, wana yafuatayo:
1. Mtu anaokolewa kwanza ndipo anajiunga na kanisa (Riggs, we Believe, p. 141).
 2. Katika katekismo yao wanasema hali hii ni Sehemu ya kanisa (p. 10).
 3. Madhehebu hayajulikani kabisa katika Agano jipya, na ni kinyume cha mafundisho yake (Mat. 15:13; 1 Kor. 1:10-13).
- G. Hawaamini kwamba ubatizo ni muhimu kwa ajili ya wokovu.
1. "Wokovu unapatikana kuititia toba kwa Mungu na imani kwa Bwana Yesu Kristo". (Statement of fundamental truths, p. 7).
 2. "Pia hufanya ubatizo kwa kutoswa ikiwa ni kwa ni utambilisho kwa waaminio hadharani uhusiano wake na Yesu Kristo pia na Mungu" (Who we are what we believe, p.22).
 3. Biblia hufundisha kwamba "ubatizo ni kwa ondoleo la dhambi" (Mdo. 2:38); "Ni kuosha dhambi" (Mdo. 22:16); ni kuingia ndani ya kanisa 1Kor. 12:13); Ni kumvaa Kristo (Gal. 3:27); na pia ni kuokolewa (Mk. 16:16; 1 Pet. 3:21).

- H. Hufanya ushirika pamoja mara moja kwa mwezi na kwenye matukio maalumu kama kwa ajiri ya shukurani, wanahuishisha na uponyaji wa mwili.
1. "Kwa imani kama tukifanyajambo lolote twaweza kuchochea uhai wa Yesu Kristo kwa njia ya uponyaji wetu: (Riggs, we Believe, p. 118,119).
 2. Biblia hufundisha kwamba chakula cha Bwana ni ukumbusho wa mauti ya Bwana (1 Kor. 11:24-26).
 3. Siku ya kwanza ya juma ndiyo siku maalumu iliyoamriwa katika Agano jipya tuchukue chakula cha Bwana (Mdo. 20:7).
- I. Wana wanawake ambao ni wahubiri, lakini Biblia imezuia wanawake kunena mbele ya kundi la watu hadharani, yaani kuwa na mamalaka juu ya wanaume (1 Tim. 2:8-15).
- J. Wanafundisha mafundisho ya uwongo kuhusu miaka elfu Premillennialism.
1. Wanafundisha kwamba wayahudi wamesharudi katika nchi ya Palestina; kwa hiyo tupo katika siku za mwisho; mpinga Kristo atatawala juu ya umoja wa mataifa; chukizo la uharibifu limekaribia; watu walio hai na walio kufa katika Kristo watakuwa katika hali ya furaha ya hali ya juu katika kipindi hicho; wale wote walio na furaha sasa watahukumiwa; "vita vya Hamagadoni" vitapiganwa katika nchi; Yesu atarudi na kuwaangamiza Wapinga-Kristo na atatawala nchi kwa miaka elfu akiwa Yerusalem. Nk. (Riggs, we Believe. Pp. 122-131).
 2. Biblia haifundishi hata mmojawapo ya hayo; inahusu juu ya kubahatisha na kupotosha unabii huu (mat. 25:31-46; Yoh. 5:28,29; 1 Thes. 4:13-5:3; Mat.16: 18;19).

Hitimisho

1. Madhehebu ya Assemblies of God ni kanisa linalikua kwa haraka sana ulimwenguni siku hizi.
2. Wana mwanzilishi asiyeh sahihi, Tarehe, na Mahali lilipoanzishwa, utaratibu na mafundisho yanayolifanya lisiwe na sifa za kanisa la ki-biblia.
3. Tutawahesabu mara zote kwamba wanastahili kufundishwa ukweli wa ijnili.

Maswali ya kujifunza.

1. Ni nini chimbuko la kanisa la Assemblies of God?
2. Ni nini waliunda ushirika wao? Wapi?
3. Nini jina la katekisimo yao.
4. Makao makuu ya kanisa la assemblies of God yapo wapi?
5. Gazeti lao la kila wiki linaitwaje? Na radio yao nayo inaitwaje?
6. Je! Kundi hili linawasadida wahubiri wengi? Ni jinsi gani kanisa hili linakufa kwa haraka? Je! Kuna washiriki wake wanaofikiri juu ya umoja wa mataifa?
7. Ni jinsi gani kanisa la Assemblies wanavyoamini kuhusu utatu wa Mungu?
8. Nini hali ya kuhusu maandiko ya Agano jipya?
9. Kanisa ki-maandiko kuhusu fundisho lao la kwamba ubatizo wa roho matakatifu uanaendelea hadi leo kwa watu wote.
10. Nini hali yao kuhusu maandiko katika Agano la kale?
11. Kanusha fundisho lao kuhusu karama za roho matakatifu kwamba miujiza inaendelea hadi siku hizi.
12. Jadiliri utaratibu wa utawala wa kanisa la Assemblies of God. Je! Unafanana na ule uliopo ndani Agano jipya?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 13-Kanisa la Nazareti

Utangulizi.

1. Madhehebu haya ni kidogo sana, lakini wanakua kidini.
2. Wana msimamo katika mafundisho, wako makini sana katika maadili na wana Juhudi katika Maisha yao.
3. Wana uhusiano na makanisa ya ki-pentecoste, lakini wanajiepusha zaidi katika hali ya ki-pentekoste.

Mazungumzo:

I. Chanzo na historia yake.

- A. Mwamko wa "Utakatifu" ulijitokeza katika karne 19 katika nchi ya Marekani.
 - 1. Lilikuwa nje ya wakati wa uamsho kupita.
 - 2. Linalezeza ya sana kuhusu usafi, kutakuwa na dhambi, kama ni kazi ya pili ya neema kuelekea katika haki.
 - 3. Historia yao ya nyuma inajengwa katika msingi wa mafundisho ya John Wesley na msukumo wa Methodist katika nchi ya Uingereza karne moja kabla.

- B. Vikundi mbalimbali nya vitakatifu vilianza kujiunga pamoja.
 - 1. makusanyiko matakatifu katika New York na majimbo New England yaliunda ushirika wa makanisa ya ki-pentekoste katika mwaka 1896.

 - 2. Katika mwaka 1895, mjini Los Angeles, CA, P.F. Bresee na J.P. Widney waliunda kwa mara ya kwanza kanisa la Nazareti lililokuwa na washiriki 135.

 - 3. Katika mwaka 1907, makundi haya yaliungana katika mji wa Chicago kwa jina la "The Pentecostal Church of Nazarene" (Kanisa la ki-Pentekoste la Nazareti).

 - 4. Kanisa la Kristo la utakatifu liliungana na Kanisa la ki-Pentekoste la Nazareti mwaka 1908.

 - 5. Makundi mbalimbali madogo katika uingereza, Scotland, na Kanada walijiunga pamoja na Kanisa la ki-Pentekoste la Nazareti.

 - 6. katika mwaka 1919, mukutano mkuu wa Madhehebu hay ulibadili jina lake kuita kanisa la Nazareti (The Church of Nazarene).

II. Ukweli wanaoufundisha:

- A. Wanaamini utatu wa Uungu.

- B. Wanaamini kuzaliwa kwa Yesu na Bikira, fidia ya kifo cha Yesu, na kufufuliwa kwa Yesu katika wafu kwa mwili wake.

- C. Wanaamini maandiko, ya kwamba yamevuvuviwa na roho.

- D. Wanaamini kwamba mtu yuko huru ki maadili kufanya mema au mabaya.

- E. Wanaamini kwamba mtoto wa Mungu, anaweza kuanguka kutoka katika neema na kupotea.

- F. Wanaamini kurudi kwa mara ya pili kwa Yesu, kiama ya wafu, na hukumu kwa ulimwengu.

- G. Wanaamini kuwa kuna mbingu na kuzimu.

III. Makosa wanayofundisha.

- A. Wana mwanzili, muda wa kuanzishwa, na Mahali lilipoanzishwa pasipo sahihi ili wawe kanisa sahihi ki-biblia (Mat. 16:18; Yoeli 2; Isa. 2; Daniel 2; Mdo. 2).

- B. Wanaamini kwamba kuna kurithi dhambi.
 - 1. "Tunaamini kwamba dhambi ya asili, ama uozo wa asili, imewaharibu wazo wote wa Adamu, kwa sababu hiyo kila mmoja amekwenda mbali kabisa ha haki au hali ya usafi wa wazazi wetu wakati ule walipoumbwa, ni uasi kwa Mungu, ni pasipo Maisha ya kiroho, na tumejifunga katika mabaya, na tunaendelea kuamini kwamba dhambi ya asili bado ipo hata

katika vizazi vipyta, hata itakapoondolewa kwa njia ya ubatizo wa roho matakatifu” (Church of the Nazarene Manual, 1976, pp. 26-27).

2. Tunahukumiwa kabla ya kutenda mema au mabaya, na tunajua tupo chini ya laana” (John Wesley, Original Sin, p. 340).
3. Kama mtu amejiharibu, moja kwa moja ni kazi ya roho mtakatifu kumwokoa.
4. Baraka ya pili au kazi ya pili ya neema huondoa hali ya dhambi za mtu.
5. Mafundisho haya yanajibowi kutoka katika neno la Mungu:
 - a. Paulo alifundisha kwamba, “kifo kiliwachukua wote, kwa sababu wote wamefanya dhambi” (Rm. 5:12), lakini wanazareti wanafundisha kwamba “dhambi imewapata wote, kwa sababu Adamu alifanya dhambi”
 - b. “Ikiwa watu wote wamezaliwa katika dhambi kwa sababu ya kosa la Adamu, halafu kuanzia kifo cha Yesu Kristo watu wote wamezaliwa wakiwa wameokolewa, Kuanzia kazi za Kristo ni kuharibu madhara ya dhambi ya Adamu. Tunalazimishwa kupokea hali hizi mbili zenye utata huenda kupotea kabisa au kiumlwengu. (Miller, why I left, pp. 126,127).
 - c. Kristo katika mwili wake alikuwa mzao wa Adamu (Luka 3:38); kulinanga na mafundisho wa wanazareti, Kristo Alikuja katika ulimwengu huu, moja kwa moja akiwa amepotea, akiwa tayari amerithi dhambi ya Adamu. Labda fundisho hili au vinginevyo mtu lazima apokee fundisho la kikatoliki kuhusu Mariamu kukingiwa dhambi ya asili.
 - d. Biblia hufundisha kwamba dhambi ni ile inayofanywa na mtu, au ambayo mtu anashindwa kuifanya, siyo kwamba mtu anairithi! (1 Yoh. 3:4; Yak. 4:17).
 - e. Hakuna kurithi dhambi, kila mtu anahusika katika dhambi yake mwenyewe (Ezekiel 18:1-4,19-20; Kumb. 24:16).
 - f. Ikiwa mtu anarithi dhambi kutoka kwa wazazi wake wasiokolewa, Je! Anaweza kuzaliwa mtoto asiye na dhambi ikiwa wazazi wake wameshapata baraka ya pili? Ikiwa mzazi mmoja ametakaswa, na mwingine hajatakaswa, Je! Mtoto atakayezaliwa atatakaswa nusu na Sehemu nyingine atakuwa amepotea?

C. Wanaamini kuwa utakaso (utakatifu ni kazi ya pili ya neema).

1. Kulingana na mafundisho ya wanazareti, mtu huenda kwa huzuni ili apokee wokovu kwa dhambi zake zilizopita.
 2. Mtu huyu tena ni lazima aende kwa huzuni ili apokee utakaso kutokana na dhambi ya Adamu; hii hufanya na ubatizo wa roho mtakatifu.
 3. “Kulingana na fundisho hili, nafsi kwanza huzaliwa na baadaye hutakaswa. Kabla ya kuchukua hali ya baraka, hii humfanya mtu kuwa mwana wa Mungu, huzaliwa, lakini huendelea kuwa aktika mfano wa mwovu” (Miller, why I left, p. 129).
 4. Biblia inatueleza kwamba, tunatakaswa kwa damu ya Yesu Kristo (Ebr. 10:14).
 5. Biblia inatueleza kuwa tumeoshwa, tumehesabiwa haki, na tumetakaswa kwa wakati mmoja l1 Kor. 6:9-11).
 6. Mtu hutakaswa, wakati anapoitii Injili (Ef. 4:24; Rum. 6:3-4, 17-18).
- D. Wanaamini kwamba kutakuwa na dhambi ni matokeo ya utakaso.

1. "Tunaamini kwamba kuingia katika utakaso ni matendo ya Mungu, linalofuata kuzaliwa, kwa hilo waaminio hufanywa huru mbali na dhambi, au upotevu, na humleta katika hali ya kujihusisha na Mungu, na hali ya utakatifu ya utii katika upendo unaomfanya mtu kuwa safi Tendo hili pia hujulikana kwa njia mbambali kama ni kuwakilisha tofauti zake kama vile ukamilisu wa Kikristo, ukamilifu wa upendo, usafi wa moyo, ubatizo wa roho mtakatifu, baraka kamilifu, na utakatifu wa kikristo". (Manual 1976 p. 29).
 2. Wanadai kwamba mtu aliyeokoka hana tamaa ya kufanya dhambi, hata hivyo wanasesma kuwa mtu anaweza kukosa na kuanguka kutoka kwenye neema!
 3. Neno "Kamili" limetumiwa katika biblia likimaanisha ukamilifu au "kukua" Filip. 3:12,13; Ebr. 6:1).
 4. Mwana wa Mungu anaweza kukosa (1 Yoh. 1:6-2:2
- E. Wanafundisha kwamba kuna utaratibu wa kuhuzunika kiroho kwa ajili ya wokovu.
1. Hotuba hutolewa ili kuwa himiza watu wanaoishi katika dhambi watubu na kuwapa uhakika kwamba Mungu atawasamehe.
 2. Wanapokuja mbele huambia kuwa wasali sala ya toba, kwa hiyo Mungu atawasamehe.
 3. Mpango wa Bwana ni tofauti kabisa na hayo (Mk. 16:15,16; Mdo. 2:38; 8:35-39; 22:16).

Hitimisho:

1. Wanao wamishenari 553 katika mataifa 60.
2. Washiriki wake katika Marekani na Kanada wanakisiwa kufikia nusu milioni, na kwa ulimwengu ni kama milioni 4.
3. Wanavyo vyuo 8 vya sana na ulegezaji, na vyuo kadhaa vingine vya kitheologia.
4. Wana nyumba yao ambayo kila utawala unatoka pale katika Kansas, Missouri.

Maswali ya kujifunza.

1. Lini, wapi, na ni nani mwanzilishi wa kanisa la Nazarene?
2. Ni lini ambapo jina "kanisa la Nazarene" lilianza kutumika?
3. Ni mambo gani ambayo kanisa la Nazarene wanayofundisha ambayo ni kweli kwa mujibu wa Biblia?
4. Kanusha ki- maandiko fundisho linalohusu kurithi dhambi.
5. Kwa nini, kufuatana mafundisho ya kanisa la Nazareti kuna baraka ya pili?
6. Ni jinsi gani Biblia inafundisha kuhusu "kutakaswa na "kuhesabiwa haki"?
7. Ni jinsi gani kanisa la Nazareti wanavyofundisha kuhusu njia ya kuokoka? Ni jinsi gani Biblia inavyofundisha?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 14-Salvation Army (Jeshi la Wokovu)

Utangulizi:

1. Kanisa la Jeshi la wokovu linategemewa sana kutokana na jinsi linavyojihuisha na kazi za jamii na kuwahurumia watu.
2. Watu wengi hawajui kwamba hili ni kanisa pamoja kwamba lina katekisimo.

Mazungumzo:

- I. Chanzo na historia yao.
 - A. William Booths ndiye mwanzilishi wa Madhehebu ya Jeshi la wokovu.
 1. Alizaliwa katika mji wa Nottigham, Uingereza mwaka 1829.
 2. Katika mwaka 1844, alikuwa mwenye uwezo wa kuzungumza na akawa mshiriki wa kanisa la Methodist.

3. akaja kuwa mhubiri wa uamsho.
- B. Mwaka 1862 alianza kufanya kazi kati ya watu maskini mjini London.
1. Mwaka 1865, Booth alianzisha huduma ya kimishieni ya ki-kristo mashariki mwa London; jina lilibadirika na kuwa Jeshi la wokovu katika mwaka 1829.
 2. Tawi la Jeshi la wokovu lilianzishwa katika Marekani mwaka 1880.
 3. Siku hizi wanachama wa Jeshi la wokovu wanakisiwa kufikia 2,000,000 katika mataifa 85.
- II. Ukweli wanaoufundisha
- A. Wanafikira ya kimaandiko kuhusu utatu wa Mungu.
 - B. Wanaamini kuvuviwa kwa maandiko.
 - C. Wanafanya Juhudi nyingi kwa kuwangalia maskini, wagonjwa, wasio na makazi, nk.
- III. Makosa wayofundisha:
- A. Katika toleo la Jeshi la wokovu lilitolewa mwaka 1899 katika mji wa New York, husema kwamba Jeshi la wokovu ni taasisi “iliyoundwa kuendesha mambo ya kidini na mashirika mbalimbali ya huruma” mabayo kusudi kuu “ni kuongoza wanaume na wanawake katika uhusiano bora na Mungu”. (What is the Salvation Army, pp. 8,9).
 - B. Utaratibu wao si kimaandiko.
1. Makao makuu yao yapo mjini London.
 2. Kichwa (Mkuu) cha jeshi la wokovu huvaa cheo cha Jenerali; wameandaa katika muundo wa kijeshi (Ef. 1:22-23; Kol. 1:18).
 3. Jenerali huongoza kuitia wafanyakazi (Mdo. 14:23; Filp. 1:1).
 4. katika nchi ya Marekani, Jeshi la wokovu limegawanyika katika wilaya nne zenye makao makuu katika New York, Chicago, Atlanta na San Fransisco.
 - a. Kila wilaya inaongozwa na kamishina.
 - b. Kamanda mkuu wa nchi ya Marekani, makao makuu yake yapo mjini New York.
 - C. Wana katekisimo yao ianyoitwa “the salvation Army handbook of Doctrine (Kitabu cha Mafundisho cha Jeshi la wokovu) (2Tim. 3:16-17).
 - D. Wanafundisha kwamba dhambi inarithiwa; wanadamu wote wamezaliwa wakiwa wamepotea. (Handbook pp. 85-86).
 1. “Mtoto mdogo” hajui jema wala baya (Kumb.1:39).
 2. Haturithi dhambi (Ezekiel 18:1-4, 19-20).
 3. Roho zetu zinatoka kwa Mungu; hivyo haziwezi kuwa na dhambi (Ebr. 12:9; Mhu. 12:7).
 - E. Wanafundisha kwamba mtu ni lazima apokeemwanga wa roho mtakatifu ndipo aelewe kuwa neno ni kweli (Handbook, pp. 89, 133). Yoh. 20:30-31; Rm. 10:17; 1 Thes. 2:13; 2 Tim. 3:16,17; 2 Thes. 2:14; Ef. 3:3,4; 2 Pet.1:3; liganisha na wokovu unavyoonekana katika kitabu cha Matendo.
 - F. Wanafundisha kuwa ubatizo siyo muhimu (Handbook, p. 185,186). (Mk. 16:16; Mdo. 2:38; 22:16; Gal. 3:3,4; 2 Pet.3:21).
 - G. Hawashiriki chakula cha Bwana.
 - 1.Wanaonya “dhidi ya hatari kuamini kila tendo la Ibada linalotoka nje ya maadili yao” (Handbook p. 88)
 - 2.Biblia hufundisha kwamba kuna ni lazima kula chakula cha Bwana kila siku ya kwanza ya Juma kwa ajili ya kumbukumbu (Mat.26:26-28; Mdo. 20:7).
 - H. Wanatumia vyombo vya muziki katika Ibada zao (Ef. 5:19; Kol. 3:16).

- I. Wana wahubiri wanawake 1 Tim. 2:8-15.
- J. Wana tafuta fedha kwa njia mbalimbali na kuongeza kutoa sadaka za hiyari (1 Kor. 16:1-2; 2 Kor. 9:6-7).

Hitimisho:

1. Jeshi la wokovu ni Madhehebu ambayo yanafundisha uwongo.
2. hayawezi kuungwa mkono wala kuhimizwa na Wakristo kwa njia ya aina yoyote 2 Yohana 1:9-11).

Maswali ya kujifunza:

1. Nani ni mwanzilishi wa Madhehebu ya Jeshi la wokovu?
2. Ni baadhi gani ya mafundisho wanayofundisha ukweli?
3. Elezea utaratibu wa Jeshi la wokovu. Uko katika maandiko?
4. Kitabu chao cha Jeshi la wokovu cha katekisimo kinaitwaje?
5. Kanusha fundisho lao ki-maandiko kwamba mtu hurithi dhambi.
6. Kanusha fundisho lao ki-maandiko kwamba mtu hawezi kuelewa maandiko mpaka aangazwe na roho mtakatifu.
7. Jeshi la wokovu wanafundishaje kuhusu ubatizo?
8. Wanafanyaje kuhusu chakula cha Bwana?
9. Wanapataje fedha kwa ajili shughuli zao? Je! Njia wnayotumia ni ya kimaandiko? Kwa nini, au kwa nini isiwe?
10. Kwa nini kutumia vyombo vya muziki ni kosa?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 15- Madhehebu ya Mennonites.

Utangulizi

1. Kuna makundi angalau 12 makubwa ya Mennonite katika nchi ya Marekani pekee na pia kuna Vikundi kadhaa vidogo vilivygawanyika kati ya hayo mikubwa.
2. Baadhi ya Wamenonites wanaonekana kiinjili zaidi kuliko Madhehebu mengine; Baadhi yao wameundwa katika Vikundi vya ki-menno zaidi kuliko vingine ambavyo vinaonekana kuwa vya kisasa zaidi.

Mazungumzo.

- I. Chanzo na Historia kwa.
 - A. Msukumo wa Ki-menonite ulikuwa kutohana na msukumo wa Ki-Anabaptist kipindi cha matengenezo ya ki-protestant.
 - B. Kusanyiko la kwanza la Menonite lifanyika katika mji wa Zurich, nchini Switzerland mwaka 1525.
 - i. Walipinga kabisa muungano wa kanisa na serikali.
 - ii. Walikana kabisa kwamba kuna ulazima wa kubatiza watoto wachanga.
 - iii. Walikataa kutoa kiapo cha utii au kutumika jeshini.
 - C. Menno Simons aliyeishi miaka ya 1496-1561, aliyekuwa kuhani (padre) wa kanisa katoliki, aliongoka katika mfumo wa kimatengenezo na baadaye akawa kiongozi; aliongoza makusanyiko mengi ambayo baadaye yalianza kuijita kwa jina lake.
 - D. Wengi walianza kuteswa na viongozi wa kanisa katoliki; na kwa ajili hii walikimbilia katika nchi ya Uingereza miaka ya 1500.

- E. Familia 13 za Ki-Menonite zilihamia katika Pennsylvania mwaka 1683.
- II. Ukweli wanaofundisha:
- A. Wanakubaliana na maandiko matakatifu, Wanakiri wazi kwamba maandiko yamevuvuviwa.
 - B. Wanafahamika sana kwa kazi zao za huruma kwa wenyewe shida, kwa kuwa wanaamini kwamba Maisha yao ya kikristo ni lazima yaambatane na kuwasaidia wenyewe shida.
 - C. Wanamini kuwa Yesu ni Mungu, na kwamba alizaliwa na Bikira, kifo chake kwa ajili ya ondoleo la dhambi, kufufuliwa katika wafu.
 - D. Wanaamini kuwa mbinguni Mahali maalumu kwa watu wema na jehanamu ni Mahali pa waovu.
- III. Makosa wanayofundisha.
- A. Wengi wa wamenonite wanapokea sala ya toba ambayo inatokana na mapokeo ya vitini 18 vilivyo sainiwa mjini Dordrecht, nchini Uhlanzi mwaka 1632 (2 Tim.3:16-17).
 - B. Wamenonite Huchukua ukumbusho wa Bwana wetu Yesu mara mbili kwa mwaka (Mdo. 20:7; Kut. 2:8).
 - C. Wamenonite wengine hubatiza kwa kumwagia maji badala ya kutoswa (Mdo. 8:38-39; Rm. 6:4; Kol. 2:12).
 - D. Wanaoshana miguu wakiunganisha na tukio la Yesu kuwaosha wanafunzi wake miguu wakati ule alipokula chakula chake na wanafunzi wake kabla ya mateso, na wao hula chakula kisha huwaosha wafuasi wao miguu.
 1. Kushana miguu ilikuwa ni desturi ya watu wa Palestina enzi zile za zamani (Mwan. 18:4; 1 Tim. 5:10).
 2. Lilikuwa ni tendo la ukaribu kwa mgeni anapoingia nyumbani kwa mwenyeji wake, na mwenyeji alionesha kumjali kwa kumwosha miguu.
 3. Yesu alionesha mfano tu wa ukarimu kwa kuwaosha miguu wanafunzi wake miguu (Yoh. 13:4-17).
 - E. Baadhi ya wamenonite, katika Juhudi yao ya kupingana na Maisha ya ulimwengu, huanza kuwazuia watu vitu vile vilivyoruhusiwa kutumika kama vile vyakula fulani nk. (1 Tim. 4:1-3; Uf. 22:18-19).

Hitimisho:

1. Makundi mawili ya Ki-Menonite katika nchi ya Marekani ni:
 - a. Mkutano mkuu wa Menonite ambao wana washiriki 100,000 katika ulimwengu mzima.
 - b. Kanisa la Menonite lenye washiriki 101,000 katika nchi ya Marekani.
2. Wengi wa wale wenyewe msimamo makali siku hizi wanapokea mageuzi.

Maswali ya Kujifunza.

1. Lini na wapi Kusanyiko la kwanza la Madhehebu ya Menonite lilikusanyika?
2. Nani ambye alionekana kuwa ni kiongozi mkuu wa Madhehebu haya na baadaye wakachukua jina lake kuwa ndio jina la Madhehebu?
3. Ni mambo gani ambayo wamenonite wanayofundisha yaliyo kweli?
4. Wamenonite wanakula chakula cha Bwana mara ngapi? Kwani kuna kosa gani kwa kufanya hivyo?
5. Wamenonite wanafanyaje wanapobatiza?
6. Kanusha kimaandiko tendo lao la kuosha watu miguu wakilinganisha wakati Yesu alipowaosha wanafunzi wake mara walapo chakula cha Bwana.

Mafundisho ya Madhehebu
Somo la 16 – Madhehebu ya Waadventist wa Wasabato

Utangulizi:

1. Hili ni kundi la kidini lililotofauti sana kihistoria mbali na Madhehebu mengine kwa jinsi wanavyodai kwamba wana mammalaka ya kuongeza chochote kwenye Biblia kwa kuwa wana uvuvio wa roho ki-unabii siku hizi.
 - a. Uvuvio inadiwa kwamba aidha upo kwa mwanzilishi au wameongezwa ufunuo mwingine zaidi kutoka kwa Mungu.
 - b. Kwa fafanuzi hizi, Kanisa la Wasabato ni Madhehebu.
2. Kanisa la Wasabato lina nguvu mno kiutendaji, ni la kiuinjilisti, na linakufa kwa haraka sana.
 - a. Ki-ulimwengu washiriki wake wanakadirwa kufikia milioni nne.
 - b. Wengi a washiriki wake wako nje ya Marekani ya kaskazini.
 - c. Wanadai kwamba wanahubiri katika lugha zaidi ya 600.
 - d. Wana mamia ya shule na hospitali kadhaa, matoleo ya vitabu na magazeti pamoja na Radio na Televisheni.

Mazungumzo:

- I. Chanzo na Historia yake.
 - A. William Miller ni mtu wa kwanza kati ya watu wawili waanzilishi wa kanisa la Wasabato.
 1. Miller, alikuwa mhubiri wa Ki-Baptist, hakuwahi kuijunga kabisa na madhehebu ya Wasabato, walakini mafundisho yake yanahuksika sana na msukumo wa madhehebu haya.
 2. Alijisumbua sana kuhusu unabii, na mwishowe alihitimisha kwamba mwisho wa ulimwengu utakuwa kati ya mwezi machi Tarehe 21, 1843 na machi 21, 1844 (Mat. 24:36). Muda huu ulipita bila kutokea kwa mwisho wa ulimwengu.
 3. Wakati unabii wa Miller ulipoonekana ni wa uwongo, mtu mwingine aliyeitwa Samuel Snow, mfuasi wa Miller, alitabiri kurudi kwa Yesu mara ya pili kungekuwa Mwezi wa kumi Tarehe 21, 1844, na Miller alikuwa na mashaka sana na hilo, hata hivyo akajifariji kwamba, asipokuja Bwana, angesikitika sana, hata hivyo pia unabii huu hakutimia pia, nao ukawa ni wa uwongo (Kumb. 18:22). Hata hivyo watu waliendelea kuwaamini, wakati huu wengine wakauza hata mali zao kwani walitegemea kuwa Yesu yu karibu na hawana sababu ya kuwa na mali, badala yake wakanunua nguo nyeupe, kama kitabu cha ufunuo kinavyosema (Uf. 7:9). Wakapanda wengine kwenye miti mirefu au milima mirefu ili wawe wa kwanza kumlaki akija mawinguni!
 4. Baada ya unabii kushindwa, wafuasi wa Miller wakasema kuwa Kristo amechelewa kwa sababu bado ameingia "Patakatifu pa patakatifu" huko mbinguni ili aanze kufanya "upatanisho wa dhambi", wakati akimaliza kazi hii, ndipo atatokea.
 - B. Ellen G. Harmon White ni mtu wa pili anayehusika na kuanzishwa kwa madhehebu haya ya Wasabato.
 1. Alipokuwa na umri wa miaka 9 alijeruhiwa vibaya na rafiki yake walipokuwa wakicheza na matokeo yake akachukuliwa na kitu kama ndoto labda kutokana na kujeruhiwa kichwani aliahirika katika ubongo.
 2. Yeye na jamii yake walijuunga na kuwa wafuasi wa Miller katika mwaka wa 1842.
 3. Katika mwaka 1844, alidai kwamba amefunuliwa mamia ya maono naufuno kadhaa kwa muda mrefu ulioendelea katika Maisha yake.
 4. Mwaka 1846, Ellen aliolewa na James White, aliyekuwa mhubiri kijana wa Miller.
 5. Kwa sababu ya uvuvio wake wa ufunuo, Alikuja kuwa kiongozi wa msukumo wa Miller, yaliozaa Wasabato.

6. Katika mwaka 1847, Ellen alidai kwamba, alipata maono, na katika hayo, alichukuliwa hadi mbinguni (linganisha na 2 Kor. 12:1-4).
 - a. Aliona Amri kumi zile za Agano la kale.
 - b. Amri ya nne (Uishike Sabato) ilikuwa imezungushiwa moto na inanga'a zaidi.
 - c. Alihitimisha ndoto yake kwamba, ni lazima watu wote waaminio washike Sabato.

C. Utaratibu wa Wasabato.

1. Katika mwaka 1860, walianza kutumia jina jipyä la Kanisa la Waadventista wa Sabato badala kufuata mpango wa Miller na Ellen akawa ndiye kiongozi.
2. Katika mwaka 1863, kulifanyika mkuu mkuu katika mji wa Battle creek, Michigan na ndipo ukawa mwanzo rasmi wa kanisa la Wasabato.

II. Ukweli wanaoufundisha.

- A. Wanamini maandiko ya Biblia, wanaamini kwamba yamevuvviwa.
- B. Wanaamini uumbaji wa Mungu kwa mujibu wa maelezo yaliyopo katika kitabu cha Mwanzo, na wanapinga mafundisho ya madiliko (evolution).
- C. Wakataza kabisa utumiaji wa kileo, tumbaku, na aina yoyote ya utumiaji wa madawa ya kulevyta.

III. Makosa wanayofundisha.

- A. Wasabato wanaamini kwamba, sheria mbili zilitolewa katika mlima Sinai:
 1. Sheria ya Mungu (yaani Amri kumi au Moral Laws) walisema kwamba hizi bado tunatakiwa kuzishika.
 2. Sheria ya Musa (the ceremonial law; yaani zile sheria ambazo zilitolewa baadaye na Musa kwa waisraeli), wanasema hizi ziliondolewa na Yesu.
 3. Biblia haioneshi aina hii ya tofauti!
 - a. Tunaposoma katika kitabu cha Nehemia 8:1,8 tunaona kuwa Ezra aliambiwa alete kitabu cha "torati ya Musa, Bwana aliowaamuru Israeli" na kisha "wakasoma katika kitabu, katika torati ya Mungu", (Chunguza kwa makini maneno yaliyotiwa wino mweusi zaidi).
 - b. Mariamu alii "torati ya Musa", ambayo iliitwa pia ni "Sheria ya Bwana" wakati ule alipompeleka Yesu kule Yerusalem kumweka kwa Bwana (zingatia kwamba sheria hiyo ya kuwaweka wakfu watoto baada ya siku arobaini tangu kuzaliwa haipo katika Amri kumi, walakini inaitwa kuwa ni sheria ya Musa na pia ni Shelia ya Bwana). (Soma Luka 2:22-23).
 - c. Sheria ile iliyoandikwa kwenye mbao mbili za mawe (yaani amri kumi ikiwemo Sabato) Mungu aliwapa waisraeli kwa mkono wa Musa, twasoma: "Tena ulishuka juu ya mlima Sinai, ukasema nao toka mbinguni, ukawapa hukumu za haki, na sheria za kweli, na amri nzuri na Maagizo; ukawajulisha Sabato yako takatifu, na kuwaagiza Maagizo, na amri, na sheria, kwa mkono wa mtumishi wako Musa". (Nehemia 9:13,14). Biblia haifanyi tofauti kabisa kwamba kuna ceremonial laws na Moral laws ni wanadamu tu ambao wanaweka tofauti hizi (gal. 1:6-9).
 - d. Sabato ilitolewa kwa waisraeli kwa sababu wao walikuwa Watumwa katika nchi ya Misri, Mungu akawapa Sabato ili wapumzike kwa kuwa utumwani hawakuwa na muda wa kupumzika, na hii wakapewa pia wawafundishe watoto wao kwamba wao walikuwa Watumwa (Kumb. 5:12-15). Je! Hawa ndugu wanaoshika Sabato leo wanafanya kwa ajili ile aliyokusudia Mungu? Je! Ellen na wafuasi

wake wao au vizazi vyao vya zamani waliwahi kuwa Watumwa nchini Misri? Hata mtanzania anaposhika Sabato leo Anawafundisha nini watoto wake kuhusu hilo analolifanya?

- e. Sheria iliyoandikwa kwenye mawe (Amri kumi) ilikuwa ni huduma iliyokuwa ikibatilika (2 Kor. 7:11) na iliondolewa na Yesu (2 Kor. 3:2-13; Rm.1-7).
- f. Kristo alikomesha torati ambayo Mungu aliitoa katika mlima Sinai, aliigongomea masalabani, isiwepo tena (Mat. 5:17, 18; Ef. 2:14-16; Kol. 2:13-17; Ebr. 7:12; 8:1-13).

B. Wasabato hufundisha kwamba Sabato (yaani siku ya saba, jumamosi), lazima watu wote kukusanyika na kumwabudu Mungu, na kwamba Mungu aliamuru tangu mwanzo, alipoumba ulimwengu, na aliitakasa mlimani Sinai.

1. Wakati Musa alipoandika katika Mwa. 2:2,3; Sabato iliyotolewa mlimani Sinai, alisema sababu, kwa nini Mungu aliwapa Sabato na kwa nini Yeye alipumnzika na kwa hali gani alifanya (Kut. 20:11).
2. Waisraeli waliamriwa kuokota mana kwa muda wa siku sita ili kuwafundisha namna ya kushika sheria itakayokuja baadaye yaani Sabato, siyo kwamba tayari walishapewa (Kut. 16:22-26).
3. Sheria ya Sabato haikutolewa siku Mungu alipomaliza kuumba ulimwengu kama wasabato wanavyosema, bali ilitolewa katika mlima Sinai. Twasoma: "Tena ulishuka juu ya mlima Sinai, ukasema nao toka mbinguni, ukawapa hukumu za haki, na sheria za kweli, na amri nzuri na Maagizo; ukawajulisha Sabato yako takatifu, na kuwaagiza Maagizo, na amri, na sheria, kwa mkono wa mtumishi wako Musa". (Nehemia 9:13,14). Pia twasoma katika Kumbukumbu 5:2-4 "Bwana Mungu wetu, alifanya Agano nasi katika Horebu. Bwana hakufanya Agano hili na baba zetu, bali na sisi, yaani, sisi sote tulipo hapa, tu hai. Bwana alisema nanyi uso kwa uso mlimani, toka kati ya moto; ..." Je! Musa na wote waliotoka Misri walikuwapo wakati Mungu alipomaliza kuumba? Sivyo! Mababa wote kuanza Adamu mpaka Musa pale sinai, yaani, kabla sheria kutolewa sinai, hawakupewa Sabato. Ni fundisho la uwongo kudai kwamba Mungu aliwapa Sabato Adamu na wale walifuata kabla ya Sinai.
4. Sabato ilikuwa ni Ishara kati ya Mungu na Waisraeli (Kut. 31:17; Kumb. 5:1-21).
5. Sabato ilikuwa ni Sehemu ya Agano la kale, iliandikwa kwenye mbao mbili za mawe, ambayo iliondolewa msalabani (2 Kor. 3:7; Kol. 2:14-17).
6. Siku ya kwanza ya Juma ndiyo siku ya kukusanyika pamoja kumwabudu Mungu, katika siku hii, wakristo wa kwanza,
 - a. walikula chakula cha Bwana, na walitoa changizo (Mdo. 20:7; 1 Kor. 16:1-2).
 - b. Kristo Alifufuka siku hii (Mat. 28:1; Marko 16:1,2).
 - c. Kanisa la Kwanza lilianzishwa siku hii (Mdo. 2:1-47; Lawi 23:15,16).

C. Wasabato hukataza ulaji wa nguruwe.

1. Hii ilikuwa ni amri ya Agano la kale ambayo ilikwisha ondolewa Lawi 11:7.
2. Kila kiumbe cha Mungu ni safi kabisa ikiwa kitapokelewa kwa shukurani (1 Tim. 4:1-5).
3. Ni dhambi kufunga sheria Mahali Mungu amefungua, Maana laichokitakasa Mungu wewe usikiite najisi (Mdo. 10:12-16; Mk. 7:20; Uf. 22:18,19).

D. Wasabato hudai kwamba Ellen G. White ni nabii.

1. “..... karama ya unabii ni moja ya kitambulisho kinachojulisha mabaki ya kanisa..... karama hii ilijulikana zaidi katika Maisha na utumishi wa Ellen G. white.” (The fundamental Beliefs of Seventh day Adventists).
2. Ilitabiriwa kwamba wakati Kristo atakapoleta wokovu kwa watu wake, karama za unabii na roho ya uchafu ingekoma (Zekaria 13:1-3); na baadaye Paulo naye alisema kuwa unabii utakoma itakapokuja iliyokamili (1 Kor. 13:8-10; 2 Tim. 3:16-17).

E. Wasabato hufundisha mafundisho ya Roho zilizolala (Soul sleeping).

1. Wanafundisha kwamba mtu kwa hali yake yote ni mfu, na hana kabisa aina yoyote ya uhai.
2. Biblia hufundisha kwamba:
 - a. Mtu aliumbwa katika hali ya mwili, nafsi na roho, (Mat. 10:28; 1 Thes. 5:23).
 - b. Roho zetu zilitoka kwa Mungu na tunapokufa roho zetu zinarudi kwake, (Mhubiri 12:7; Zekaria 12:1; Ebr. 12:9).
3. Maelezo ya Yesu kuhusu tajiri na Lazaro katika Luka 16 unakanusha fundisho lao la “roho zilizolala”.
 - a. Wengine husema “huu ilikuwa ni mfano tu”
 - i. Biblia haikusema kwamba huu ulikuwa mfano
 - ii. Hata kama ungekuwa ni mfano, mifano ya Yesu siku zote ilielezea na kusimamia mambo yaliyokuwa kweli (Mat. 13:10-15).
 - b. Yule tajiri alikuwa na fahamu zake, alimtambua Lazaro, na alikumbuka kwamba anao ndugu watano katika nchi (Luka 16:23-28).

F. Wasabato wanakataa mafundisho ya Biblia kwamba kuna adhabu ya milele katika moto kwa wasiotii.

1. Wanaamini kwamba Shetani na wasioamini watatoweza wasiwepo tena.
2. Motoni na mbinguni kwa maneno mengine inaonekana inafanana kwa upana ulio sawa (Mat. 25:46).

Hitimisho.

1. Kanisa la wasabato lina mwanzilishi asiye sahihi, Mahali na Tarehe zisizo sahahihii, na mafundisho yasiyo sahihi kulifanya liwe kanisa la Agano jipya.
2. Matendo yao yote mazuri hayatakuwa na maana ikiwa hawatafanya mapenzi ya Mungu (Mat. 7:21-23).

Maswali ya Kujifunza

1. Mahdhehebu ni nini? Je! Wasabato ni madhehebu? Kwa nini?
2. Ni akina nani hasa wanahuksika moja kwa moja na kuanzishwa kwa madhehebu haya?
3. Unaweza kukumbuka alichokitabiri William Miller kuhusu Kristo? Ilitimia? Yesu alisema nini kuhusu hilo?
4. elezea maono ya Ellen G. White alivyopelekwa mbinguni. Alielezea alichokiona huko mbinguni? Je! Mtume Paulo aliruhusu watu waige hilo?
5. Kanusha kimaandiko fundisho la Wasabato kuhusu kuwapo sheria mbili zilizotolewa Sinai.
6. Kanusha kimaandiko fundisho la wasabato kwamba sisi tunawajibika kuabudu siku ya jumamosi (yaani, siku ya Sabato). Thibitisha kama tunatakiwa kuabudu siku gani.

7. Kanusha kimaandiko madai ya Ellen kwamba alikuwa na karama ya unabii.
8. Kanusha kimaandiko mafundisho ya wasabato kuhusu "Roho zilizolala".

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 17 – Madhehebu ya Kanisa la Kristo la watakatifu wa siku za mwisho (Mormons).

Utangulizi:

1. Kanisa la Mormon ni moja ya taasisi ya kidini inayokuwa kwa haraka zaidi ulimwenguni nyakati hizi.
2. Imekuwa moja ya madhehebu mpya inayodai kwamba wanauvvvio wa nje ya Biblia.
 - a. Kitabu hicho kilichovuvviwa nje ya Biblia ni Kitabu cha Mormon.
 - b. Ni mafundisho na maagano.
 - c. Kuna vito vya thamani kubwa.
3. Ni taasisi tajiri sana.
4. Vijana wanategemewa kujitoa angalau kwa miaka miwili katika Maisha yao kwa kazi ya kimishieni wakisaidiwa na jamii zao.

Mazungumzo:

- I. Chanzo na Historia yao:
 - A. Joseph Smith alianzisha Kanisa la Mormon huko Fayette, New York Tarehe 6 April 1830.
 - i. Wakati akiwa na umri wa miaka 14, Smith alidai kuwa malaika alimtokea na kamwambia kuwa asijiunge na kanisa lolote lililokuwepo wakati ule.
 - ii. Miaka machache baadaye malaika akamwongoza mpaka Mahali ambapo alikuta sahani ambazo kitabu cha Mormon kilitafsiriwa.
 - iii. Alianza kutafsiri sahani zile mwezi septemba, 1827 na kumalizika mwezi Agosti 1829.
 - iv. Smith pia laidai kuwa Yohana Mbatizaji alimtokea na Oliver Cowdery akawa kuhani Mahali pa Haruni.
 2. Baadaye walisema kuwa Petro, Yohana na Yakobo waliwapatia ukuhani wa Melikizedeki na funguo za utume.
 - B. Upinzani uliwalazimisha Smith na wafuasi wake kukimbilia Mahali mbambali.
 1. Mwaka 1831, Walianzisha makao makuu huko Kirtland, Ohio.
 2. Baadaye waondoka Mahali pa uhuru, katika Missouri, lakini waliondolewa katika 1839.
 3. Ndipo wakaa huko Nauvoo, Illinois.
 4. Joseph Smith na ndugu zake walifungwa huko Carthage, Illinois mwaka 1844, Joseph akauawa na kundi la watu wengi mwezi Juni 27, 1844.
 - C. Kwa ajili ya kutafuta uongozi (ukuu) kulisababisha Magawanyiko.
 1. Joseph Smith, Jr. alitambuliwa kama rais wa kanisa la Mormon, lililoweka makao makuu huko Independence, Missouri.
 2. Brigham Young aliongoza kundi kubwa la Wamormon hadi Utah Mahali walipojenga hekalu huko Salt lake City.
- II. Ukweli wanaofundisha:
 - A. Wanafundisha kuwa kila mtu anahusika katika dhambi yake na siyo kwamba mtu anarithi toka kwa Adamu.

- B. Wanafundisha kwamba ubatizo ni wa kutoswa na kwamba ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi.
- C. Wanaamini kwamba chakula cha Bwana ni lazima kiliwe kila siku ya kwanza ya juma.
- D. Wanafundisha kwamba kila mshiriki ni lazima awe mmishenari.
- III. Makosa wanayofundisha.
- A. Wanakosea kuhusu hali na asili ya Mungu.
1. Kama kuna mtu ana makosa katika hatua hii, basi haijalishi ni kiasi gani anafundisha ukweli katika mafundisho yake mengine, maana hayatakuwa na msingi (Ebr. 11:6).
 - a. Wamormons so wakristo kwa namna ya aina yoyote kwa sababu ni watu wanaoamini miungu wengi (Polytheists).
 - b. Biblia hufundisha kwamba kuna Mungu mmoja tu (1 Tim. 2:5; Ef. 4:6; Yak. 2:19).
 2. Biblia hufundisha kuwa kuna nafsi tatu za Mungu zilizotofauti zinazokamilisha Mungu mmoja.
 - a. Baba ameitwa kuwa ni Mungu. (1 Kor. 8:6).
 - b. Mwana ameitwa Mungu (Yohana 1:1-3; Ebr. 1:8)
 - c. Roho Mtakatifu ameitwa Mungu (Mdo. 5:3,4).
 3. Wamormon hufundisha kwamba kila kitu chenye kuvu za kimiujiza ni miungu. (“katika hali yake ya kufa, mtu ni mungu katika kwa asili yake”. James Talmage, Article of faith, P. 530).
 4. Wanafundisha kwamba, Adamu, Ibrahimu, Isaka, Yakobo na wengine wameshakuwa miungu. (The doctrine and Covenants, 132:19;20).
 5. Wamormon wanafundisha kwamba Mungu ana mwili wa kawaida kama wa Binadamu.
 - a. “Baba ana mwili wa nyama na mifupa inayoweza kukamatika kama aliyvo Mwanadamu.....” (The doctrine and Covenants, 130:22).
 - b. Biblia husema Mungu ni Roho (Yoh. 4:24); na Roho haina mwili na mifupa kama wanadamu (Lk. 24:39).
- B. Wanafundisha kwamba utume bado upo na unaendelea hadi leo, hivyo wana baraza la mitume kumi na mbili ambalo ndilo mwamuzi wa mwisho.
1. Ili mtu awe mtume ni lazima awe amemwona Yesu baada ya kufufuka kwake (Mdo. 1:22).
 2. Hii ndiyo sababu alimtokea Yesu kule njiani alipokuwa akienda Dameski (Mdo. 22:6-16).
 3. Hakuna Mwanadamu hata mmoja anayeishi siku hizi ambaye alimwona Yesu aliyefufuka katika wafu.
- C. Wanafundisha kwamba karama za miujiza bado zipo pamoja ufunuo vinaendelea.
1. Ufunuo wao siku hizi umebadirika, zamani waliamini kuwa watu weusi si watu ila ni Wanyama, walakini sasa wamebadirika kwa shinikizo la hali ya kisiasa dhidi ya weusi.

2. Karama za miujiza zilikoma baada ya Agano jipya kukamilishwa kuandikwa (I Kor. 13:8-13; Yak. 1:25).

D. Wamormon wana vitabu vingine vilivyovuviwa wakiongeza zaidi ya Biblia.

- i. Biblia imekamilika haihitaji nyongeza. (2 Tim. 3:16,17).
 - ii. Hata kama ni malaika akisema neno lolote liliotofauti na Biblia haturuhusiwi kumwamini (Gal. 1:6-9).
2. Biblia ina kila kitu tunachokihitaji katika Maisha ya utauwa. (2 Pet. 1:3).

E. Kitabu chao cha Wamormon kinaitwa kimevuvuviwa kimejaa makosa mengi.

1. Kulingana na Alma 7:10, Yesu alizaliwa Yerusalem, lakini Biblia inasema kwamba, alizaliwa Bethlehem (Lk. 2:4-7).
2. Waamini walijiitwa wakristo siku nydingi kabla ya kuzaliwa Yesu kulingana na Alma 46:15; lakini Biblia inasema kwamba “wanafunzi walianza kuitwa wakristo kwanza huko Antioquia” (Mdo. 11:26b).
3. Wanasema kwamba Yesu alionekana katika dunia baada ya kupaa kwake akiwahudumia watu kulingana na III Nephi 10: 18,19; lakini Biblia inafundisha kwamba, atakuwepo mbinguni mpaka wakati wa kurudi kwake mara ya pili duniani, na kila jicho litamwona na hata wale waliomchoma (Mdo. 1:11; 3:20,21; Uf. 1:7; Ebr. 10:12,13).

F. Wamormon wanafundisha kwamba watu leo wanweza kuchukua ukuhani wa Melikizedeki, lakini Yesu Kristo ni kuhani wetu mkuu, mtu pekee aliye kuhani milele kwa mfano wa Melikizedeki (Ebr. 5:5-10).

G. Wamormon hubatiza ubatizo wa wafu.

1. Wanasema vibaya 1 Kor. 15:29
2. Mafundisho yao huwapa waamini wao nafasi ya pili kuokolewa, walakini biblia inakataa. (Luka 16:19-31; Ebr. 9:27; 2 Kor. 5:10).
3. Ili mtu abatizwe wa mujibu wa maandiko, ni lazima kwanza asikie neno la Mungu (Rm. 10:17; 10:14; 44,45; Ebr. 8:11; Mdo. 16:32).
4. Ili mtu abatizwe wa mujibu wa maandiko, ni lazima kwanza aamini kuwa Yesu ni mwana wa Mungu (Mk. 16:16; Yoh. 8:24; Ebr. 11:6; Mdo. 16:31).
5. Ili mtu abatizwe wa mujibu wa maandiko, ni lazima kwanza atubu dhambi zake (Lk. 13:3; Mdo. 2:38; 17:30-31).
6. Ili mtu abatizwe wa mujibu wa maandiko, ni lazima kwanza amkiri Yesu mbele ya watu (Mt. 16:16; 10:32,33; Mdo. 8:37; Rm. 10:9,10).
7. Mtu aliyekufa hawezi kusikia, kuamini, kutubu au kuungama, kwa hiyo mtu aliyekufa hawezi kubatizwa.
8. Amri hizi ni zinamhusu mtu binafsi, na zimelenga kwa mtu mwenyewe na si kwa niaba ya.

Hitimisho.

1. Wamormon Wanadai kuwa wanabatiza watu kwa ondoeo la dhambi, lakini ubatizo wao si wa kimaandiko maana msingi wake si wa kimaandiko. Kwani Hawaamini Mungu wa Biblia bali mungu wao wenyewe kweli akili zao.
2. Wamormon wanafanya ndoa za kiroho, mume na mke katika Maisha haya ya duniani wakioana, basi wamefungwa kwa Maisha ya milele (Mt. 22:29,30; Rm. 7:1-3).
3. Kuanzia mwaka 1876, Wamormon hafanyi ndoa za mitala, lakini hata hivyo mitala ni Sehemu ya mafundisho yao (Mat. 19:4,5).
4. Wamormon wanataji kumjua Mungu wa kweli ili waokolewe. (Yoh. 17:3).

Maswali ya kujifunza

1. Kwa nini madhehebu ya Mormon si kanisa?
2. Kwa nini Mmormon hawezi kuitwa mkristo kwa namna yoyote ile?
3. Nani alianzisha dini ya Wamormon? Lini? Ni wapi alidai kwamba amepata mamalaka?
4. Kanusha kimaandiko fundisho la Wamormon kuhusu Mungu.
5. Kanusha kimaandiko fundisho la Wamormon kuhusu kuendelea kwa utume hadi siku hizi.
6. Kwa nini ni kosa siku hizi kuendelea kwa ufunuo wa unabii?
7. Kanusha kimaandiko fundisho la Wamormon kuhusu ubatizo wa wafu.
8. Kwa nini hata ingawa Wamormon wanabatiza kwa kutoswa na kwa ondoeo la dhambi bado si ubatizo wa kimaandiko?
9. Ni lazima Wamormon wamjue nani ili waokolewe?

Mafundisho ya Madhehebu

Somo la 18 – Madhehebu ya Kanisa la Mashahidi wa Yehova (Jehovah’s Witness).

Utangulizi:

- 1.Haya ni moja ya madhehebu mmojawapo ya yale ya aina ya kiunabii yaliyopo hivi sasa ulimwenguni.
 - a.Kila mshiriki anawajibika kwa kazi ya kuhubiri mlango kwa mlango imani yao.
 - b.Wanatumia mno katika kazi yao ya kuhubiri maandiko waliyoya chapa na wana bidii ya hali juu kuyasambaza.
- 2.Mwaka 1985, Mashahidi wa Yehova ilidiwa kwamba walikuwa wakifikia idadi ya milioni mbili na nusu.
 - a.Zaidi ya 600,000 wako katika nchi ya Marekani.
 - b.Washiriki wao wamepatikana katika nchi zaidi ya 216.
 - c.Zaidi ya wamishenari 6,000 wamefundishwa.
- 3.Matoleo yao na ugawaji wao kwa kawaida ni hali ya juu sana.
 - a.Gazeti la Mlinzi (Watchtower) limeenea sana na inakadirwa kiasi cha nakala zaidi ya milioni kumi zimesambazwa.
 - b.Zaidi ya nakala bilioni moja zimesambazwa katika lugha 176 kuanzia mwaka 1920.
- 4.Mashahidi wa yehova hujisingizia kwamba wao ni kanisa la Bwana.
- 5.Watu wa Mungu ni lazima kujifunza Juhudi yao katika kusambaza maandishi yao na mfano wao wa kuhubiri nyumba kwa nyumba.

Mazungumzo:

- I. Chanzo na Historia yao.
 - A. Charles T. Russell alianzisha magazeti ya mlinzi na kutoa vipeperushi kuhusu Biblia.
 1. Russell alikuwa mchungaji wa kanisa la Wasabato katika kusanyikao la Allegheny, Pennsylvania.

2. Mwaka 1879, alianza kutoa magazeti ya Sayuni mlinzi na akawa na mshiriki hasa wa Kristo.
 3. Aliandika matoleo sita kati ya saba yalihusu kujifunza katika maandiko.
 4. Alitabiri kwamba Yesu atarudi mwaka 1914.
 5. Russell alikufa mwaka 1916.
- B. Mwamuzi Joseph F. Rutherford, mwanasheria mshauri wa magazeti ya mlinzi, alimrithi Russell kama kichwa cha taasisi hii.
1. Mwaka 1920, Rutherford aliandika kwamba mamilioni ya watu wanaoishi siku zake hawatakuwa hata atakapokuja Yesu.
 2. Alitabiri, "Kwa hiyo tuna hakika kutegemea kwamba mwaka 1925 tuona ishara ya kurudi kwa Ibrahim, Isaka, na Yakobo na manabii waaminifu wa zamani....." (Mat. 24:36; Kumb. 18:22).
 3. Rutherford alikufa mwaka 1942 na Nathan Knorr akawa raisi Mahali pake.
 4. Fredrick franz kwa kawaida alihudumu akiwa kama kichwa cha taasisi hii.
 5. Ki-ulimwengu Makao makuu yapo Brooklyn, New York, Marekani.

II. Ukweli wanaoufundisha:

- A. Wanafundisha kwamba kila mshiriki ni mtumishi, kwa hiyo ni lazima ajitoe kuhubiri habari za ufalme.
 - B. Wanaelewa kwamba ubatizo ni wa kutosa walakini wanakosa namna wanavyoolewa kusudi la ubatizo.
 - C. Wanaamini kuwa maandiko ya Biblia yamevuvuwa na roho mtakatifu.
1. Hata hivyo wanayo tafsiri yao ianyoitwa "tafsiri mpya ya ulimwengu" ambayo inalenga kuelezea mafundisho yao.
 2. Kila mwamini ni lazima awe na gazeti la mlinzi kama ufunguo wa kufungua maandiko.
 3. Kwa hiyo wanafuata jamii ya mlinzi wanavyosema kwamba maandiko yana maana gani, na si kwamba, ni kitu gani hasa maandiko yanasema.

III. Makosa wanayofundisha.

- A. Mashahidi wa Yehova wana makosa kwa jinsi wanavyofundisha kuhusu asili ya Mungu.
 1. Kwa sababu ya hili, mfumo wao wote hauna msingi! (Ebr. 11:6; Yoh. 8:24; 17:3).
 2. "Nini, Je! Kuna ukweli wowote unaonenesha utatu?" Wala neno, hata wazo katika maneno ya Mungu, Biblia. Mafundisho haya kuanzishwa na Mungu." (The truth that leads to Eternal life, P.25).
 - a. Kile ambacho mashahidi na wengine hukiita utatu Biblia hukiita "Uungu". (Mdo. 17:29; Rm. 1:20).
 - b. Ni bora kutumia namna maandiko yanavyosema kuliko kutumia wazo linalojionesha katika maandiko.
3. Biblia hufundisha kwamba kuna Mungu mmpja tu. (Kumb. 6:4).

- a. "Theos" ni jina la Kiyunani (Kigiriki) linaloonesha asili ya Mungu. Kuna Mungu mmoja tu kwa asili, Hivyo, kuna Mungu mmoja tu. Hata hivyo kuna nafsi tatu zinazofanya kuwepo na Mungu mmoja, yaani Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" (Guy N. Woods, commentary on James, p. 139).
 - b. Uungu unaonekana katika mistari ifuatayo: (Mat. 3:16,17; 28:19; 2 Kor. 13:14).
4. Baba anaitwa Mungu. (Ef. 4:4-6).
 5. Mwana ameitwa Mungu. (Yoh. 1-3; 10:30; 20:28; Flp.2:5-9; Kol. 2:9; Ebr. 1:8).
 6. Roho Mtakatifu naye ameitwa Mungu. (Mdo. 5:3,4).
 7. Kwa ufupi ni kwamba, tunaposema kuwa kuna nafsi tatu za Mungu, hatuna maana kwamba, kuna miungu watatu, la hasha, bali, Mungu katika hali yake amedhihirika katika hali tatu. Twaweza kutoa mifano machache kujaribu kuelezea hali ya Mungu: Ikiwa mtu anaweza kufananisha Uungu wa Mungu na familia, atakosea sana, Mungu hayuko kama vile familia ilivyo, yaani, Baba, mama na mtoto, ukweli ni kwamba hawa ni watu watatu waliotofauti kabisa, ingawa wanaishi kwa kutegemeana, walakini kimawazo, kimwili, na hata haki za msingi kiroho wanatofautiana. Kwa hiyo Uungu wa Mungu ni tofauti na familia. Labda, twaweza umaja wa Mungu na mama mijamzito akiwa na mwanawe tumboni, wanashirikiana kila kitu ambacho mama anakula ndicho alacho na mtoto, walakini bado wao no tofauti kabisa, kwani mmoja anaweza kufa bila ya mwingine kuathirika. Je! Nafsi tatu za Mungu zinahusiana vipi ili awe Mungu mmoja?

Jibu la swalii hili laweza kueleweka kama ifuatavyo: Mungu ni kama mtu mmoja lakini ana sehemu zake tatu, yaani, mwili, Roho na mawazo ya yake. Kila Sehemu ya mtu yule ni muhimu ili awe Yeye hasa, na ukiondoa Sehemu moja wapo basi mtu huyu hawezi kuwa mtu tena. Kwa mfano; ikiwa mtu ni mzima, walakini akili yake ina matatizo, twaweza kumwona mtu huyu ni mzima? Labda mwili wake umeharibika kabisa, twaweza kusema mtu huyu ni mzima? Labda roho yake imeondoka ndani ya mtu twaweza kusema mtu huyu ni mzima?

Vivyo hivyo; na Uungu wa Mungu ndivyo ulivyo; si kwamba kuna miungu watatu bali kuna Mungu mmoja, bali ana Sehemu zake tatu ambazo ni: Baba, mwana na Roho.

8. Tangu Kristo ameitwa mzaliwa wa kwanza wa kuumbwa kwa ulimwengu; Mashahidi wahoji kwamba, yeye Kristo aliumbwu kwanza, ndipo Mungu akaendelea kuumba vitu vingine (Kol. 1:15).
 - a. Wazo la kiyunani hapa lilifasiriwa "mzaliwa wa kwanza" lina maana kwamba, ni katika hali ya kuonesha mwanzo, au mtangulizi katika jambo lolote. (Kol. 1:18).
 - b. Ni kama katika ufunuo 3:14, Kristo anaitwa "mwanzo wa kuumba kwa Mungu".
 - i. Hapa mashahidi hudai kwamba, inaonesha kuwa Mungu alianza kumwumba Yesu kabla ya viumbi vingine.
 - ii. Neno la kiyunani lilitumiwa katika ufunuo ni ($\alpha\rho\chi\eta\varepsilon$) "Arche" lina maana ya "asili" yaani, Tunaweza kusema, uumbaji wa Mungu asili yake ni Yesu, na pasipo yeye hakikufanyika kilichofanyika (Yohana 1:3).

B. Mashahidi wa Yehova Wanakosea wanapo zungumza kuhusu ufalme.

1. Wanafundisha kwamba ufalme ulikuja mwaka 1914. Wanahesabu kutoka katika kitabu cha Daniel ambaye alisema kuwa ufalme ungekuja siku 2520 zitakapotimia, Wanadai kuwa tangu mwaka 606, wakati ufalme wa nyumba ya Daudi ulipokomeshwa na mfalme wa Babeli, hadi mwaka 1914 ni miaka 2520 na wanasesma kuwa siku moja ni sawa na mwaka mmoja. Walakini hilo lina shida kwa sababu, kitabu cha Daniel hakielezi wazi siku hizo, pia fafanuzi ya siku moja ni kama mwaka mmoja haipo katika Biblia; ila ni kwamba; siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja kwa Mungu (2 Pet. 3:8).

2. Zaidi ya hivyo Biblia inafundisha kama ifuatavyo:
 - a. Isaya alitabiri kwamba ufalme utaanzishwa Yerusalemu katika siku za Mwisho. (Isa. 2:1-4).
 - b. Yoeli alisema kwamba Roho itamwangwa kwa wote wenye mwili katika siku za mwisho huko Yerusalemu na wokovu utapatikana kwa watakao amini (Yoeli 2:28-32). Je! Watu hawakuokolewa kabisa kabla ya 1914? (Soma Mdo. 2:47; Kol. 1:13-14).
 - c. Daniel alitabiri kwamba ufalme ungekuja katika siku wanapotawala Warumi (Dan. 2:1-45; Lk. 3:1-2; Mdo. 2:1-47).
 - d. Yohana alihubiri akisema "Tubuni, kwa maana Ufalme umekaribia". Maana yake ufalme wa Mungu ulikuwa umekaribia sana wakati ule Yohana Mbatizaji alipokuwa akihubiri. (Mat. 3:1,2).
 - e. Yesu mwenyewe pia alihubiri akisema kuwa Ufalme umekaribia (Mk. 1:14,15).
 - f. Yesu alifundisha kwamba, baadhi ya wanafunzi wake ambao alikuwa nao wakati ule, wasingekufa hata wauone ufalme umekuja kwa nguvu. (Mk. 9:1). Je! Mitume wa Yesu waliendelea kuwa hai hadi mwaka 1914?
 - g. Yesu aliahidi kujenga kanisa lake, ambalo ndilo ufalme wake, pia akaahidi kumpa Petro funguo za ufalme wa mbinguni (Mat. 16:18,19). Je! Ina maana kwamba, Petro alikuwa hai hadi 1914 ili afungue ufalme watu waingie?
 - h. Nguvu za Roho mtakatifu zilikuja siku za mwisho katika Yerusalemu juu ya mitume, na wokovu kwa waaminio ulipatikana siku ile ya Pentekoste, hivyo watu waliingga katika ufalme. (Mdo. 2:1-47).
 - i. Kuanzia siku ya Pentekoste na kuendelea, ufalme unaelezwa kuwa tayari umeshakuja. (Mdo. 8:12; Kol. 1:13; Uf. 1:6,9).
 - j. Kwa hiyo ufalme ambao ni kanisa, ulikuja mwaka 33 BK. Na si 1914.

C. Mashahidi kukosa katika fundisho lao la kurudi kwa Yesu mara ya pili.

1. Wanafundisha kwamba kurudi kwake Yesu mara ya pili kulifanyika mwaka 1914, lakini kwa siri ambako kulikuwa si wazi kwa Mwanadamu kumwona. (From Paradise lost to Paradise regained, p. 174).
2. Biblia hufundisha kwamba, hakuna mtu ajuaye siku wala saa ya kuja kwake Bwana. (Mat. 24:36; Mk. 13:32-33; 1 Thes. 5:1-3).
3. Biblia hufundisha kwamba kurudi kwake Bwana kutakuwa wazi kwa kila jicho na hata wale waliomchoma (1 Thes. 4:16; Mdo. 1:9-11; Uf. 1:7).

D. Mashahidi hukosea katika mafundisho yao kuhusu asili ya mtu.

1. Wanasema kwamba mtu hamiliki nafsi ila yeye mwenyewe ni nafsi. (The truth that leads to eternal life, p. 36).
2. Wanafundisha kwamba mara mtu anapokufa na nafsi yake pia hufa. (The truth that leads to eternal life, p. 37).
3. Biblia hufundisha nini juu ya jayo?
 - a. Mtu ameumbwa na Mungu katika hali ya mfano wake; Mungu ni roho, na roho haina mwili wala mifupa, kwa hiyo, mfano wa Mungu ambao upo kwa mtu ni roho yake, siyo mwili. (Mwa. 1:26,27; Yoh. 4:24; Lk. 24:39).
 - b. Mtu ameumbwa katika hali tatu, nazo ni Mwili, Nafsi, na Roho. (Mdo. 5:23; Mat. 10:28).
 - c. Nafsi wakati mwingine husimama badala ya mtu mwenyewe binafsi. (Mdo. 7:14).
 - d. Nafsi na Roho ni vitu viwili tofauti, lakini wakati mwingine hutumiaka pamoja au kwa kubadilishana. (Ebr. 4:12).

- e. Wakati mtu anapokufa, mwili wake hurudi katika mavumbi, lakini roho yake hurudi kwa Mungu aliyeitoa. (Muhubiri 12:7; Zekaria 12:1; Ebr. 12:9).

E. Mashahidi hukosea katika mafundisho yao kuhusu Jehanamu.

1. Wanakana kwamba kuna moto wa milele.

- a. Jehamu, wanasema, ni kaburi tu. "Watu wema kama vile watu wabaya wote huenda Jehanamu ambayo ni kaburi la kila mtu". (The truth that leads to eternal life, p. 42).
- b. Watu wote wanaohubiri kwamba watu watakwenda Jehanamu, mashahidi huwaita "Wahubiri wa Jehanamu. (Let God Be True, p. 76).

2. Biblia inafundisha nini juu ya Jehanamu?

- a. Jehanamu kwa mujibu wa Biblia ni Mahali ambapo roho za wasiotii zitakaa zikisubiri siku ya kufufuliwa. (Lk. 16:19-31; 23:42-43; Mdo. 2:27-31; 2 Pet. 2:4).
- b. Ni Mahali pa mateso ya milele (Mat. 10:28; 25:41,46; Mk. 9:43-48; Uf. 20:14; 21:8).
- c. Jehanamu siyo Mahali pa ndoto tu kama mashahidi wasemavyo, bali ni Mahali palipo wazi na pa milele kama vile mbingu ilivyo.

F. Mashahidi wana makosa kwa sababu wanakana kufufuliwa kwa mwili wa Bwana wetu Yesu katika wafu.

1. Mashahidi hufundisha kwamba, "Mfalme Kristo Yesu alikuwa kifo cha mwili na alifufuka katika mwili usioonekana, yaani ulikuwa ni wa kiroho....." (Let God Be true, p. 122).

2. Biblia inasema nini?

- a. Ufufuo wa Yesu ulithibitisha kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu (Rm. 1:4).
- b. Kama Yesu hakufufuka, imani yetu ni upuuzi. (1 Kor. 15:12-19).
- c. Tomaso aliamini pale alipothibitisha ufufuo kwa kupapasa vidonda nya Yesu nya mwili wake. (Yohana 20:28429).
- d. Mwili wa Yesu uliwekwa kaburini ijumaa jioni, jumapili asubuhi mwili wake haukuwepo, ni hakika Yesu alifufuka. (Lk. 23:50-55; 24:1-3).
- e. Hotuba ya Petro katika matendo 2:27-32, alikuwa akithibitisha maneno ya manabii kwamba "mwili wa mtaktifu Yesu haukuona uharibifu". Ni nini hicho kinachoitwa uharibifu? Bila shaka ni mwili wake uliwekwa kaburini na si roho yake, yaani, alikaa kaburini na kabla hajaoza alifufuka asioze.

Hitimisho.

1. Mashahidi wa Yehova hufundisha mafundisho mengi ambayo ni uwongo, ni machache tu ambayo tumeyaeleza hapa.
2. Mashahidi hawana fundisho lolote la kutosheleza kuhusu dhambi au kifo cha Yesu kwa ajili ya dhambi za watu.
3. Kama tulivyo sema hapo juu wana makosa kuhusu mambo ya milele, wao wanasema kuwa milele ni hapa duniani tu (2 Pet. 3:10-12; Ebr. 1:10-12; 2 Pet. 3:13).
4. Mashahidi wa Yehova, kama vile madhehebu mengine wote, wanatakiwa wafundishwe ukweli ili waokolewe.

Maswali ya kujifunza.

1. Nani alianzisha madhehebu ya Mashahidi wa Yehova? Nani alikuwa mrithi wake?
2. Gazeti lao mashuhuri linaitwaje? Ni kiasi gani limezunguka dunia?
3. Ni jinsi gani Mashahidi wa Yehova wanakua kwa haraka? Watu wa Mungu wanaweza kujifunza lolote kwao?

4. Kanusha kimaandiko fundisho la Mashahidi kuhusu Asili ya Mungu.
5. Ufalme ulianza lini kwa mujibu wa Mashahidi? Biblia inasema nini kuhusu kuanzishwa kwa ufalme?
6. Kanusha kimaandiko fundisho la Mashahidi kuhusu Asili ya Mtu.

*Mungu na akubariki uwe mwaminifu kuwafundisha madhehebu wautambue ukweli ili waokolewe.
(Ndugu Makanyaga JM, BRS, 2002; Csop; Chimala Mbeya; Tanzania).*

*Notes Written By Rod Rutherford
Translated by John Makanyaga*